
Jumatano Septemba 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581810
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



**RODRI SASA KUKOSA MSIMU MZIMA CITY**

UKURASA 21

**Polisi** yachunguza kifo kijana akiwa kwenye matibabu

UKURASA 2

**Kortini** madai kutapeli kwa kutumia jina la Kikwete




UKURASA 7

**SMZ** yanunua ndege zisizo abiria ukaguzi hifadhi misitu




UKURASA 17

# 1,800/- zilivyowezesha watoto kupata mchele, nyama, mafuta kupikia

UKURASA 3



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akipokea zawadi ya pesa kutoka kwa mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Chief Zulu, baada ya kuizindua shule hiyo, mjini Songea mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## WAFARIKI DUNIA KUNYWA KITU KINACHOHISIWA KUWA NA SUMU

UKURASA 3

## Viongozi na wanachama CHADEMA waachiwa huru

# TAMISEMI yaomba siku 14 kiapo kinzani uchaguzi Serikali za Mitaa

UKURASA 2



MICHEZO YANGA YAIGEUKIA KENGOLD LIGI KUU UK.24 MAONI, UK.6

# TAMISEMI yatakiwa kuwasilisha kiapo kinzani siku 14 mahakamani

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo Dar es Salaam, imetoa siku 14 kwa upande wa Jamhuri kuwasilisha kiapo kinzani katika kesi ya kikatiba iliyofunguliwa na wanaharakati watatu kupinga Wizara Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo, baada ya kutoa kibali kwa Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, Mwenyekiti wa JUKATA, Dk. Annanilea Nkya na Bubelwa Kaiza cha kuwasilisha mapitio ya mahakama (Judicial review) ili kutekeleza haki kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Kesi ilitajwa jana mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu, David Ngunyale, jopo la mawakili wa serikali liliomba lipewe siku 14 kuwasilisha kiapo kinzani kwa ajili ya kujibu hoja zilizowasilishwa na wanaharakati hao kupitia mawakili wao Mpare Mpoki na Jebra Kambole.

Hata hivyo, Wakili Mpoki na Kambole walipinga hoja hiyo kwa madai kuwa wamewasilisha mapitio hayo chini ya hati ya dharura, kwa upande wao siku hizo ni nyingi.

Jaji Ngunyale alikubaliana na ombi la upande wa Jamhuri la siku 14 na kuahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 7, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa, kama kila kitu kitakuwa kimewasilishwa kwa wakati mahakamani hapo, basi kesi itasikilizwa.

Wanaharakati hao, wamefungua kesi hiyo dhidi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Wangwe na wenzake wanapinga uchaguzi huo kusimamiwa, kuratibiwa na kundeshwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI, badala yake Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), kwa mujibu wa Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi ya mwaka 2024.

Pia, wanapinga kanuni za uchaguzi huo za mwaka 2024 zilizotungwa na Waziri wa TAMISEMI, wakihoji mamlaka yake ya kutunga kanuni hizo.

Awali, mahakama hiyo ilikataa kutoa zuio la utekelezaji wa mchakato wa uchaguzi unaoendelea hivi sasa kwa sababu waleta maombi hawakuweka hoja hiyo kwenye kiapo chao wala kwenye maelezo yao ya shauri walilokuwa wamefungua.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 umepangwa kufanyika Novemba 27.

Agosti 15, 2024 Waziri wa TAMISEMI alitangaza kuanza kwa mchakato wa uchaguzi huo kuanzia tarehe hiyo hadi Novemba 27, mwaka huu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza kwenye mkutano kuhusu ajenda ya upatikanaji wa nishati, ulioandaliwa na Taasisi ya Global Energy Alliance for the People and Planet (GEAPP), katika makao makuu ya Taasisi ya Rockerfeller, jijini New York, Marekani, juzi. **PICHA: OWM**

# NGO zasaidia kupunguza ndoa, ukeketaji wa watoto

**Na Elizabeth Zaya,** TARIME

UWAPO wa taasisi na mashirika ya kutetea haki za watoto wilayani Tarime mkoani Mara, umesaidia kupunguza ndoa za utotoni na vitendo vya ukeketaji kwa wasichana, imeelezwa.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wlaya ya Tarime, Peragia Baron, alisema hayo jana alipozungumza na viongozi kutoka Mtandao wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni (TECMN) unaounda zaidi ya mashirika 80 likiwamo la Msichana Initiative, walioko katika ziara maalumu wilayani hapa kutoa elimu kwa jamii kuwalinda watoto dhidi ya ndoa za utotoni.

Alisema miaka ya nyuma hali ya ndoa za utotoni wilayani hapa ilikuwa juu kwa sababu watoto wengi walikuwa wanaozwa wakiwa wadogo baada ya kukeketwa.

"Ndoa za utotoni zipo na zinaendelea na zamani mtoto alikuwa akifika darasa la nne, analipiwa mahari na inaeleweka kabisa kwamba ni mke wa mtu na akiifika darasa la saba anaolewa," alisema.

Alisema kwa desturi za wakazi wa Tarime, mtoto akitahiriwa au kukeketwa huhesabiwa ni mtu mzima, hivyo anafaa kuoa au kuolewa.

"Sasa hivi hizo ndoa za utotoni bado zipo lakini si kwa kiwango kikubwa sana kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Kuna baadhi ya sababu zilizochangia kupungua ikiwamo ujio wa vituo kwa taasisi za kutetea haki za binadamu vinavyosaidia kulea watoto wanaokimbia kuozwa kama hivi vya Masanga.

"Kwa hiyo napendekeza kuongezeka kwa mashirika kama haya hata huko vijijini ili wafikiwe na elimu hii, kwamba programu zinazotolewa na mashirika haya zikifika kila kijiji, kwa asilimia kubwa tunaweza kuwaokoa wasichana wasiingie kwenye ndoa hizo za utotoni kwa sababu wengi hawana elimu huko na hawajui wakatoe taarifa wapi," alisema.

Baron alisema maeneo yanayoongoza kwa kasi kwa mimba za utotoni na ukeketaji ni ya mipakani kama Sirari na Nyamongo ambayo yana shughuli nyingi za biashara ya madini.

Alisema sababu kubwa kinachochangia mimba za utotoni katika wilaya hiyo ni vitendo vya ukeketaji na kwamba inapofika msimu wa ukeketaji kituo cha Masanga huwa kinaelemewa kutokana na kupokea wasichana wengi wanaokimbia kukeketwa.

Baron alisema kila mwaka wamekuwa wakitenga bajeti maalumu kwa idara ya ustawi wa jamii kwa ajili ya uelimishaji kuhusu kupambana na vitendo hivyo vya ukeketaji na ndoa za utotoni.

Lilian Kimati, Mratibu wa Mtandao wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni Tanzania, alisema lengo la kutoa elimu hiyo wanatamani ndoa hizo ziishe ili watoto wapate fursa ya kutimiza ndoa zao.

"Ndiyo maana tumekuwa tukipigania sana mabadiliko ya sheria ya ndoa ambayo inatoa mwanya kwa watoto wadogo kuolewa, tunaamini hii ikifanyiwa mabadiliko huenda ndoa hizi za utotoni ikabaki historia," alisema.

Hivi karibuni Shirika la Msichana Initiative lilieleza kusikitishwa kwake kutokana na kukwama kwa mchakato wa kufanyia mabadiliko vifungu vya 13 na 17 vya sheria ya ndoa ya mwaka 1971 vinavyoruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa. Valerian Mgani, Meneja Miradi wa Association for Termination of Female Genital Mutilation (ATFGM) Masanga wilayani Tarime, alisema juhudi zote wanazozifanya kupambana na ndoa hizo za utotoni wilayani humo zimekuwa zikikwamishwa na baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kuwalinda wale wanaotekeleza vitendo hivyo.

"Sisi tunapofanya kazi kupambana na vitendo vya ukeketaji pamoja na ndoa za utotoni, tunaingia kwenye vita kali na baadhi ya wanasiasa, wao wanasema eti tunaingilia mila za wapigakura wao na hata tukiwapeleka polisi wanaona tunakwenda kinyume na taratibu zao, wanapambana kuwatoa," alisema Mgani.

Kwa mujibu wa Utafiti wa Demografia na Afya (TDHS) wa mwaka 2015/16, asilimia 36 ya wasichana Tanzania wanaolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 huku mikoa inayoongoza kwa ndoa hizo ikiwa ni Shinyanya asilimia 59, Tabora asilimia 58, Mara 55 na Dodoma 51.

## Polisi yachunguza kifo cha kijana aliyefariki akiwa katika matibabu

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, limesema linachunguza kifo cha utata cha Johnson Josephat, maarufu kama Sonii (39), Mkazi wa Unga Limited, jijini hapa, anayedaiwa kufariki dunia, baada ya kutoroshwa na kundi la watu waliokuwa wakipinga kukamatwa kwake baada ya kufungwa pingu mkono mmoja.

Josephat alifariki dunia juzi akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Justine Masejo, alisema Septemba 23, muda wa saa 11:30 jioni, askari polisi ambaye hajatajwa jina wala namba yake ya kijeshi, alifika maeneo ya Unga Limited kwa ajili ya kumkamata mtu huyo kwa madai ya kuhusika kwenye tukio la kuvunja stoo na kuiba.

"Lakini wakati wa ukamataji askari alifanikiwa kumvisha pingu mkono mmoja, ndipo lilipojitokeza kundi la watu na kumshambulia askari, kumkamata mtu huyo na kumtorosha kwa kutumia pikipiki," ilidai taarifa ya polisi iliyotolewa kwa umma jana.

Kwa mujibu wa SACP Masejo, taarifa za awali zinaonesha kuwa katika harakati za kumtorosha mtuhumiwa huyo alianguka na baadaye ndugu walimpeleka hospitalini lakini alifariki.

Uchunguzi wa tukio hilo unaendelea ili kubaini chanzo cha kifo hicho ikiwamo kuchukua hatua kwa waliohusika ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mke wa marehemu, Nasra Bakari, akizungumza katika video iliyosambaa mtandaoni, alisema mumewe alimkuta amekanyagiwa kichwa chini na askari wawili wa polisi.

Alipouliza chanzo chake, aliambiwa kuna mtu mmoja alikuwa amekamatwa na polisi kwa tuhuma za wizi wa compreser, na alimtaja marehemu kuwa ni mhusika.

Alisema baada ya kutajwa na polisi kumkamata mumewe walianza kimshambulia akiwa na pingu mkononi hadi kupoteza fahamu.

Kwa mujibu wa Nasra, walipomkimbiza Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mount Meru, walikataliwa mgonjwa wao kutibiwa kwa sababu alikuwa na pingu mkononi.

HABARI KITAIFA

# 1,800/- zilivyowezesha watoto kupata mchele, nyama, mafuta

**Jenifer Gilla na Gideon Mwakanosya**

KATIKA hali isiyotarajiwa, wanafunzi wa awali katika Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Chief Zulu, katika Mtaa wa Namanyigu Kata ya Mshangano, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, walimpa Rais Samia Suluhu Hassan Sh. 1,800 walizochanga kwa nyakati tofauti.

Baada ya Rais Samia kufika shuleni hapo, mwanafunzi mmoja alikwenda moja kwa moja na kumpa Sh. 50.

Akisimulia tukio hilo ambalo alionyesha lilimgusa, Rais Samia alisema mwanafunzi alipokea fedha hiyo kisha akamrudishia lakini baada ya kutafakari, aliamua kumtafuta na kuipokea tena.

"Nilivyomtafuta nikampata nikamwambia nipe ile pesa uliyotaka kunipa. Akanipa kisha nikaona wanafunzi wenziwe nao wanakuja kunipa Sh. 50 na 100. Nilipohesabu baadaye nikajikuta nina Sh. 1,800," alisema.

Rais Samia alisema alimchukulia mtoto huyo kama malaika aliyekwenda kumpa baraka, ndiyo sababu iliyomsukuma kumtafuta na kuzipokea fedha zote. Alisema hali hiyo ilimfurahisha na kumtafakarisha, hivyo kuamua kuwapa ng'ombe wawili, mchele kilo 500 na mafuta ya kupikia.

"Sasa hizi fedha nakwenda kuziweka kwenye makumbusho yangu na maandishi maalum ya watoto hawa. Kama wajukuu, wamepata fikra ya kunigawia mimi bibi. Kwa nini mimi bibi nisiwagawie wao," alisema.

Rais aliwahimiza walimu wa shule hiyo wawatunze na kuwalinda watoto hao na majengo ili yaendelee kuwa na hali hiyo na kuvutia kwa muda mrefu.

### MAZAO YA BIASHARA

Akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa maghala 28 ya kuhifadhi nafaka katika kijiji cha Luhimba, Rais aliwakumbusha wakulima kuwa na matumizi mazuri ya fedha ili soko la mazao linaposhuka wasiathirike kiuchumi.

Aliwakumbusha wakulima wa kahawa kuongeza jitihada katika uzalishaji ili kukuza uchumi na hatimaye serikali ijiepushe na misaada na mikopo yenye masharti.

Rais pia aliweka jiwe la msingi katika mradi wa maji wa Mtyangimbole, kijiji cha Madaba na kutembelea shamba la kahawa la Aviv Tanzania, kijiji cha Lipokela.

Akiwa kijijini hapo, Rais aliwasihi wakulima wa mazao yote nchini kuwa na mipango mizuri ya matumizi ya fedha ili wasishuke kiuchumi kwa kuwa soko la mazao lina tabia ya kupanda na kushuka.

"Kwa hiyo niwaombe sana wakulima wote, misimu ikiwa mizuri bei ikiwa nzuri, tujue kujiwekea akiba ili mabadiliko ya tabianchi yakituathiri, mvua zisipokuja, bei zikishuka, tusiteteleke kiuchumi na hali za maisha," alisema.

Rais aliwasihi wakulima wa kahawa kuongeza kasi ya uzalishaji ili nchi ijitegemee kwa kuwa fedha zinazotumika kuboresha sekta ya kilimo, likiwamo zao hilo.

Alisema kama nchi itakuwa na uwezo wa kuzalisha dola milioni 250 na zaidi kwa kahawa pekee, huku wakulima wakiongeza juhudi na kuzalisha zaidi, nchi itaondokana na mikopo yenye masharti.

"Tunapotaja dola milioni 250 ndugu zangu, huwa nakwenda nje napiga magoti, nabembeleza na kuomba na wakati mwingine kwa masharti," alisema.

Rais alimwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kushughulikia malalamiko ya wananchi ya kukatwa fedha kinyemela na vyama vikuu vya ushirika na kuweka mfumo wa uwazi ili wanufaike na mazao yao.

Pia aliwakumbusha wakulima wa kahawa wazingatie uhifadhi wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazosababisha mvua kutotabirika ili wawe na uhakika katika uzalishaji wa mazao yao.

Rais Samia aliitaka Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) kufuata masharti yanayoyotolewa na soko la Ulaya ya kutokukata misitu kwa ajili ya kulima kahawa kwa kuwa wakifanya hivyo, zao hilo halitanunuliwa.

Alisema Umoja wa Ulaya (EU) ulielekeza kuwa mashamba yote mapya yatambuliwe na kusajiliwa katika soko la dunia ili kufahamu kahawa imetoka mashamba yapi na kama kuna uharibifu wowote wa mazingira.

"Hili nalo si la kupuuza. Naomba twende nalo tuliandikishe ili tusije tukakosa soko zuri la kahawa kule Ulaya," alisema.

Rais alielekeza teknolojia ya visima vya umwagiliaji, kilimo cha pilipili manga na paprika iliyoko kwa mwekezaji ipelekwe kwa wananchi ili nao waitumie kwenye kilimo na kujiongezea kipato.

Pia alisema tangu nchi ipate uhuru, serikali imeanza kutoa ruzuku kwenye zao hilo hali iliyosababisha kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 65,000 hadi 80,000 nchi nzima na kuongeza kipato kupitia fedha za kigeni na mwaka huu, mauzo ya kahawa yanatarajia kuingiza dola milioni 250.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, serikali ilipunguza makato ya tozo na ushuru, ukiwamo ushuru wa halmashauri kutoka asilimia tano hadi tatu ili mkulima afurahie kazi ya mikono yake.

### SERIKALI ZA MITAA

Akiwa Peramiho, Rais Samia aliwasisitiza wananchi kujitokeza kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba, mwaka huu, kugombea nafasi mbalimbali na kuwachagua viongozi wanaofaa.

Aliwasihi kuchagua wagombea wa Chama Cha Mpinduzi (CCM) kwa sababu serikali yake inawajibu wa kuhakikisha nchi inabaki salama na utulivu wa kisiasa na kuwaletea maendeleo.

Rais pia aliwataka Watanzania kudumisha amani, utulivu na usalama katika maeneo yao kwa kuwa ndio msingi wa maendeleo ya nchi na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuwaletea maendeleo.

Aliwaeleza Masista wa Shirika la Masista Wamisionari Wabenediktini wa Tutzing kudumisha upendo kwa watu wote bila kuangalia utofauti za dini kwa kuwa binadamu wote ni sawa na hakuna mtu aliyeumbwa tofauti na mwenzake.

Waziri wa Kilimo, Bashe alisema kuwa ujenzi wa maghala 28 Luhimba ni sehemu ya kwanza ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia ya kujenga maghala 70 vijijini yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1000 kila mojawapo yatakayogharibu Sh. bilioni 14.7 sawa na Sh. milioni 527 kwa kila ghala.

Alisema kuwa maghala hayo yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Songea Manispaa na idadi ya magahala kwenye mabano ni Songea Mji, Songea DC (11), Madaba (9) na Namtumbo (saba).

Bashe alisema maghala mengine ni Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) matano kuhudumia wakulima na kati ya 28, mengine matano yanatarajiwa kukamilika wiki chache zijazo.

Alisema NFRA pia itajenga maghala makubwa ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua tani 5,000 kila ghala katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Ruvuma, Songwe na Tabora.

### TAMISEMI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema ujenzi wa Shule ya Msingi Chief Zulu uliogharimu Sh. milioni 626.43 ulibuniwa na madiwani wa halmashauri hiyo.

Awali, Waziri wa Afya na Mbunge wa Peramiho, Jenista Mhagama, alimwomba Waziri Bashe aongeze miradi ya umwagiliaji ili kuboresha mazao ya kilimo cha biashara katika eneo hilo.

**Rais aliwahimiza walimu wa shule hiyo wawatunze na kuwalinda watoto hao na majengo ili yaendelee kuwa na hali hiyo na kuvutia kwa muda mrefu.**

## Viongozi, wanachama wote CHADEMA waachiwa huru

**Jenifer Gilla**

VIONGOZI na wanachama wote wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waliokamatwa wakati wanajiandaa na maandamano ya amani juzi wameachiwa na polisi.

Chama hicho kiliandaa maandamano ya amani kuomboleza wenzao waliofariki dunia katika mazingira tatanishi, kupinga vitendo vya utekaji, utesaji na mauaji ya viongozi na wanachama wa chama hicho.

Hata hivyo, maandamano hayo yalipingwa na Jeshi la Polisi na kutoa onyo kwa wananchi kutoshiriki kwa madai kuwa hayapo halali, hata hivyo baadhi ya viongozi na wanachama walikaidi agizo hilo na kwenda maeneo walioelekezwa kwa ajili ya kuandamana.

Katika tukio hilo, baadhi ya viongozi waliokamatwa ni Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu, Mwenyekiti wa chama Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema na Naibu Katibu Mkuu Bara, Benson Kigaila.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema kuwa viongozi wote wa chama hicho waliachiliwa kwa dhamana mpaka kufikia jana.

"Ndio nimefika sasa hivi lakini nimetaarifiwa kuwa mpaka leo hakuna kiongozi yeyote wa chama aliyepo polisi wote waliachiwa jana kwa dhamana," alisema.

Aidha, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje CHADEMA, John Mrema, alimweleza mwandishi kuwa wanachama wote waliokamatwa katika harakati za maandamano hayo wameachiwa na polisi.

Juzi usiku viongozi wa CHADEMA waliachiwa na polisi lakini waligoma kuondoka kwenye vituo hadi wanachama wao wote walioshikiliwa watakapoachiwa.

Aidha, Jeshi la Polisi jana lilizingira ofisi za chama hicho zilizopo Mikocheni, Dar es Salaam na ya Kanda ya Pwani iliyopo Kinondoni, Mtaa wa Ufipa.

Taarifa iliyowekwa katika mtandao wa kijamii wa X wa chama hicho jana ilieleza kuwa wakati polisi wakizunguka nje ya ofisi za Mikocheni ndani ya jengo kulikuwa na baadhi ya viongozi wakiendelea na majukumu yao.

Viongozi hao ni Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA), Catherine Ruge, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA), Yohana Kaunya, Mkuu wa Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo wa chama, Julius Mwita na maofisa wengine wa chama.

Septemba 11, mwaka huu, chama hicho kiliwataarifu Watanzania kuwa kingefanya maandamano hayo Septemba 23, mwaka huu kama mpaka Septemba 21 serikali isingeonyesha mwanga wa kushughulikia maagizo walioyatoa.

Mbowe alitaja maagizo hayo kuwa ni kuwataka Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni na viongozi waandamizi wa vyombo vya ulinzi na usalama wa Jeshi la Polisi na Usalama wa Taifa wajiuzulu kama sehemu muhimu ya uwajibikaji.

Alisema pia waliagiza kurejeshwa kwa viongozi wao waliotekwa kwa zaidi ya mwezi mmoja, wakiwa hai au wamefariki, wakiwamo Katibu Mwenezi wa Sumbawanga Mjini Dionise Kipanya, Katibu wa Chama Wilaya ya Temeke, Jacob Mlay, Katibu Mwenezi, Muheza Tanga, Mbwana Kombo.

Alisema pia waliitaka serikali kuruhusu uchunguzi huru utakaofanywa na wachunguzi huru kutoka Scotland Yard ya Polisi kutoka nchini Uingereza kwani vyombo vya usalama vya nchini ni sehemu ya washukiwa.

Alisema ndani ya miezi mitatu viongozi sita wa chama hicho walitekwa katika mazingira ya kutatanisha likiwamo tukio la kutekwa na kuuawa kwa Mjumbe wa Sekretarieti ya chama hicho taifa, Ally Kibao, Septemba 7, kisha mwili wake kukutwa ukiwa umetupwa Ununio, Tegeta, Dar es Salaam Septemba 8, mwaka huu, ukiwa na majeraha.



Katibu wa Bunge, Baraka Leonard (kulia), akikabidhiwa rasmi ofisi na aliyekuwa Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi. Makabidhiano hayo yamefanyika jana katika ofisi ya Bunge, jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wafariki dunia kunywa kitu kinachohisiwa kuwa na sumu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU wawili wakazi wa Picha ya Ndege, Kibaha mkoani Pwani, wamefariki dunia baada ya kunywa kimiminika kinachodhaniwa kuwa na sumu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, aliwaambia waandishi wa habari jana ofisini kwake mjini hapa kuwa taarifa ya tukio hilo ilitolewa juzi saa 4:00 asubuhi.

Kamanda Lutumo alisema baada ya kupokea taarifa hiyo, walifuatilia na kubaini kuwa Septemba 20, mwaka huu, Humphrey Kayombo (44), Deogratius Agustino (49) na Abas Yohana (48) wakazi wa Picha ya Ndege, walifika kwa Edwin Kavishe mfanyabiashara wa vyakula na vinywaji wakiwa na kinywaji chao.

Kwa mujibu wa Lutumo, watu hao wakiwa na kinywaji hicho kilichokuwa kwenye chupa ya plastiki ya maji safi, walikunywa kwa kushirikiana.

"Katika hali isiyo ya kawaida, Septemba 21, mwaka huu, watu hao kwa nyakati tofauti walianza kupata maumivu ya tumbo na macho hali iliyosababisha kupelekwa Hospitali za Rufani ya Mkoa ya Tumbi na Lulanzi kwa matibabu.

"Hata hivyo siku hiyo hiyo, majira ya saa 10:00 jioni, Kayombo alifariki dunia akiwa anaendelea na matibabu," alisema.

Kamanda Lutumo alisema Septemba 22, mwaka huu, Agustino naye alifariki dunia, hivyo kusababisha hali ya shaka kuhusu vifo vyao hali iliyowalazimu kutoa taarifa Jeshi la Polisi na uchunguzi ukaanza.

Alisema Yohana naye anadaiwa kupata maumivu makali ya tumbo na macho na alitibiwa katika Hospitali ya Lulanzi kisha kuruhusiwa kurudi nyumbani akiwa na tatizo la kuona kwa shida.

Lutumo alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kwa uchunguzi wa kitaalamu kubaini sababu za vifo na madhara ya kiafya.

Abas ambaye anadai kwa sasa amepoteza nguvu ya kuona, alisema siku ya tukio, wakiwa katika sehemu ya vinywaji eneo la Picha ya Ndege, walifika vijana wawili wanaowafahamu wakiwa na chupa za maji na walipowauliza walisema wameweka kinywaji aina ya K-Vant.

"Nikanywa glasi ya kwanza nikaona kama pombe kweli lakini nikaona mbona sijaielewa kama ni K- Vant kweli. Nikaweka glasi nyingine nikachanganyia na soda nikaweka na pale nilikuwa na kijana mwenzangu anaitwa Kayombo na Deo niliwakuta tulikuwa wengi tukaendelea kunywa.

"Kulikuwa na kinadada wengine ambao walitudhihirishia kwamba pombe hiyo haina shida. Walikunywa pombe hiyo na kusema ni nzuri, mimi nikawa nakunywa kidogo kidogo,"alisema.

Abas alisema hali yake ilibadilika na kwenda kutibiwa hospitalini kisha baadaye kuruhusiwa lakini mpaka sasa haoni.

Naye Baraka Ibrahim ambaye aliyekunywa kinywaji hicho, alisema yeye ndiye aliyempeleka Abas hospitalini na aliporudi usiku, kichwa kilianza kumuuma na kuona kiza na baadaye hakuwa na nguvu ya kuona tena.

Alisema ni mara ya kwanza kunywa kinywaji hicho na kwamba aliyewaletea aliwapatia tu na yeye hakunywa.

# Mradi wa TAHA kusamehewa kodi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kutoa msamaha wa kodi kwa mradi wa Feed the Future Tanzania unaofadhiliwa na Marekani na kutekelezwa na Asasi Kilele inayojishughulisha na kilimo cha mboga, maua, matunda na viungo (TAHA).

Mradi huo unalenga kupunguza upotevu wa chakula baada ya kuvuna kutoka asilimia kati ya 30 na 40 hadi asilimia 15 kwa mazao ya mboga na kutoka asilimia 13 hadi asilimia saba kwa nafaka ifikapo mwaka 2028.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alisema mchango wa serikali katika mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 50 ni pamoja na kuondoa ushuru kwa chochote kitakachonunuliwa.

"Hatua hii itausaidia mradi kuwahudumia wakulima kwa gharama nafuu," alisema Mweli jijini Arusha muda mfupi kabla ya kuzindua maonesho ya siku mbili ya teknolojia za uhifadhi na uongezaji thamani wa mazao baada ya kuvuna.

Alibainisha njia za kufikisha teknolojia kwa wakulima zikiwamo kupitia kutoa msamaha wa kodi, ruzuku na kupitia mikopo ya taasisi za fedha.

Pia alisema ukosefu wa teknolojia unafanya mazao mengi yapotee baada ya kuvuna, lakini pia kuharibiwa na wadudu na hivyo kuziweka afya za walaji hatarini.

"Upoteaji wa mazao baada ya kuvuna unapaswa kujumuisha wadudu kuharibu mazao ambayo kimsingi hayapaswi kuliwa," alisema Mweli.

Alisema kupitia teknolojia mkulima mwenye ekari 10 za zao la alizeti anaweza kununua mashine ya Sh. milioni 3 na kukamua mafuta ya kupikia ya kutosha kusambaza katika jamii inayomzunguka.

"Hatuwezi kuendelea kuagiza mafuta ya kupikia toka nje kila mwaka wakati malighafi zote za kuchakata alizeti tunazo," alisema Mweli na kuongeza kuwa serikali imeamua kuviwezesha vikundi vya wakulima kuchakata mafuta ya kupikia.

Kutokana na serikali kutoa ruzuku ya mbegu bora za alizeti mwaka 2022, uzalishaji wa zao hilo umeongezeka toka tani 490,000 hadi kufikia tani trilioni 1.1.

Takriban kampuni 30 zilipiga kambi katika viwanja vya Makumbusho ya Azimio la Arusha zikionesha teknolojia mbalimbali zikiwamo za kubaini afya ya udongo, uvunaji, uhifadhi, uchakataji, ufungishaji na uongezaji thamani ya mazao.

Mweli alisema miongoni mwa changamoto zinazozikumba nchi za kiafrika katika kilimo, Tanzania ikiwamo, ni pamoja na gharama za uzalishaji kuzidi zile za sokoni na hivyo kuisababishia hasara sekta hiyo.

Kwa sababu hiyo serikali, pamoja na mambo mengine, imewekeza kwenye kubaini afya ya udongo, ili kuongeza tija katika kilimo.

Kiongozi Mkuu wa Mardi wa Feed the Future Tanzania, Amani Temu, alisema kuanzia mwakani maonyesho hayo yatafanyika mkoa kwa mkoa, ili kuwafikia watumiaji wa teknolojia hizo waweze kuvuna na kuongeza thamani ya mazao.

Alisema mradi utajikita katika kukuza uhifadhi wa chakula, uchakataji mazao na ufikiaji wa masoko ya kikanda na yale ya kimataifa.

Pia alisema mradi utajikita katika utatuzi na uchechemuzi wa changamoto za kisera ili mashine za kuhifadhi na kuongeza thamani ya chakula zipatikane kwa bei rafiki.

"Tutafanya kazi kwa karibu na wadau mbalimbali serikalini na sekta binafsi kuhakikisha changamoto za kisera zinapata ufumbuzi na upotevu wa mazao baada ya kuvuna unaendelea kupungua hata baada ya mradi kwisha," alisema Temu.

Katibu Mkuu huyo alisema serikali imeithibitisha TAHA kutekeleza mradi huo kutokana na kuwa historia inayotukuka katika sekta ndogo ya mbogamboga nchini.

"Tutakuwa wanafiki kama tutakiongelea kilimo cha mbogamboga bila kuitaja TAHA. Japo kilimo hicho kilikuweko kabla, likini taasisi hii imetoa mchango mkubwa kukifikisha kilipo," alieleza.

Akimkaribisha Katibu Mkuu kuzindua maonesho hayo, Mtendaji Mkuu wa TAHA, Dk. Jacqueline Mkindi, aliishukuru ofisi yake na wizara kwa ujumla kwa kuendelea kuiaminni TAHA na kuisaidia sekta ndogo ya mbogamboga nchini.

Aidha, aliishukuru serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Kimataifa la Maendeleo (USAID) kwa kuijengea msingi sekta ndogo ya mbogamboga wakati inaanzishwa na kuendelea kuilea hadi sasa.

"Tunajivunia usafirishaji na huduma nyingine za kampuni tanzu ya TAHA, TAHAFRESH, kwa sababu USAID walishiriki kujenga," alisema Dk. Mkindi.

# EWURA yazileta mamlaka nishati nchini

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imechaguliwa kuwa mwenyeji wa vikao vya kamati ndogo za Umoja wa Mamlaka za Udhibiti wa Sekta ya Nishati Kusini mwa Afrika (RERA) kwa mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na EWURA, lengo mahususi la mikutano ya RERA ni kuwezesha taasisi wanachama kubadilishana uzoefu wa udhibiti na utendaji wa sekta ya nishati katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Ilisema mamlaka za udhibiti kutoka Angola, Botswana, Afrika Kusini, Namibia, Lesotho, Eswatini (Swaziland zamani), Zambia, Malawi, Msumbiji, Zimbabwe na Tanzania zimeshiriki vikao hivyo ambavyo vilianza rasmi juzi Zanzibar hadi 27, mwaka huu.

"Vikao hivyo vinavyoendelea visiwani Zanzibar, vinaangazia masuala mbalimbali ikiwamo namna ya kuboresha shughuli za udhibiti wa nishati katika maeneo ya fedha, rasilimali watu, huduma kwa wateja, habari, mawasiliano na teknolojia ya habari, bei, tozo na viwango vya huduma kwenye sekta za umeme, mafuta na gesi asilia," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imeshiriki kama mtazamaji kwa kuwa bado haijawa mwanachama rasmi wa umoja huo.

Pia ilisema mikutano ya RERA inafanyika kwa awamu mbili, na kwamba ya kwanza ni ngazi ya watendaji, ambao wanaketi katika vikao vya kamati ndogo sita, kati ya muda uliotajwa, na ngazi ya wakuu wa taasisi wanachama wa RERA, ambao vikao vyao vitafanyika kuanzia Oktoba nane hadi 11, mwaka huu.

**Taarifa hiyo iliongeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imeshiriki kama mtazamaji kwa kuwa bado haijawa mwanachama rasmi wa umoja huo.**

# PM: Tanzania kuwa mwenyeji mkutano wa nishati Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa masuala ya nishati barani Afrika utakaotafuta namna ya kukusanya Dola za Marekani bilioni 190 ili zitumike kufikisha umeme kwa wananchi milioni 300 barani humo ifikapo mwaka 2030.

Hatua hiyo inatokana na mkakati wa serikali kupeleka umeme vijijini na vitongojini kwa kasi hali ambayo imezivutia taasisi za Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kuamua kufanya mkutano huo mkubwa ifikapo Januari, 2025.

"Wameridhishwa na utendaji kwenye sekta ya nishati, wameridhishwa na mkakati wa serikali wa kupeleka umeme mpaka vijijini, sio tu vijijini, lakini mpaka kwenye kila nyumba. Wameamua kuitisha mkutano mkubwa barani Afrika ambao utawakutanisha wadau mbalimbali, taasisi za kimataifa na taasisi zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali na kampuni ili waweze kuwekeza kwenye umeme."

Waziri Mkuu, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa kujadili ajenda ya upatikanaji wa nishati Afrika ulioandaliwa na Taasisi ya Global Energy Alliance for People and Planet (GEAPP) jijini New York, Marekani.

Akizungumza na washiriki wa mkutano huo uliofanyika kwenye ofisi za taasisi ya Rockefeller, alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa baraka zake ili Tanzania iwe mwenyeji wa mkutano huo.

Alisema mkutano huo ambao utaendeshwa kwa pamoja baina ya WB, ADB na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, unatarajiwa kuwaunganisha viongozi wa dunia, wataalamu kutoka viwandani, asasi za kiraia katika kutafuta namna ya kuwezesha upatikanaji wa nishati za uhakika, teknolojia bora za nishati safi na sera endelevu.

"Ninaipongeza Serikali ya Norway na Taasisi ya Rockefeller kwa kuamua kuunga mkono jitihada za Benki ya Dunia na ADB za kuhakikisha umeme unapatikana kwa watu milioni 300 ifikapo mwaka 2030. Mpango huu ni wa muhimu hasa kwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambako watu zaidi ya milioni 600 hawana fursa ya kupata umeme. Hatuwezi kuwa na maendeleo endelevu kama hatutashughulikia kwa haraka changamoto hii," alisema.

Alizishukuru Benki ya Dunia na AfDB kwa ahadi yao kuwa wataendelea kushirikiana na serikali ili kufanikisha mkakati wa Tanzania wa kupeleka umeme kila nyumba uwe umekamilika ifikapo 2030.

Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina, alisema wanawake milioni 900 wanataabika kwa kukosa nishati safi ya kupikia na kila mwaka ilhali upishi unapaswa uwe ni wa staha. "Wanawake milioni 130 wanatakiwa wawe wamefikiwa na huduma hii kila mwaka. "Tunapoteza wanawake na watoto wengi kwa sababu ya kukosa huduma hii."

Dk. Adesina alimpongeza Rais Samia kwa kusimamia vema sekta ya nishati na hasa uzalishaji wa nishati safi ya kupikia na kwamba anataka kuona ifikapo mwaka 2030, malengo ya kuhama kutoka kupikia kuni na mkaa kwenda nishati safi yawe yametimia.

Wakati huohuo, Rais wa Liberia, Joseph Boakai ambaye alishiriki kikao hicho, alisema umeme ni suala muhimu kwenye maisha ya mwanadamu na linapaswa kupewa kipaumbele kikubwa kwa kuwa bila umeme hakuna maendeleo.

Alisema nchini Liberia ni asilimia ndogo tu ya nchi hiyo ndiko wanapata umeme na tena kwenye maeneo ya mji mkuu.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alisema Tanzania inaungana na mataifa mengine ambayo yanaunga mkono mkakati wa hatuna haja ya kumwacha mtu nyuma katika suala zima la ujenzi wa kesho iliyo bora kwa vijana.

Ametoa kauli hiyo wakati akichangia mada kwenye mjadala wa The Future Starts Now uliokuwa sehemu ya kuhitimisha mkutano wa siku mbili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Kujadili Hatima ya Siku Zijazo (Summit of the Future) ulioanza juzi kwenye makao makuu ya Umoja wa Mataifa, jijini New York, Marekani.



Mafundi wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mkoa wa Mara, wakitandaza mabomba kwa ajili ya kupeleka huduma ya maji, katika Kijiji cha Nyegina, Kata ya Nyegina, Musoma Vijijini, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# India/JKCI kuwajengea uwezo watoa huduma kwa teknolojia

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Medanta ya India, imesema ipo tayari kushirikiana na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), kuwajengea uwezo watoa huduma hususan madaktari bingwa pamoja na wauguzi, ili kutumia teknolojia mpya ya matibabu ya kisasa iliyopo duniani.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Medanta, Idara ya Magonjwa ya Moyo na Bingwa wa Magonjwa hayo, Dk. Praveen Chandra, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema Medanta inakusudia kutoa mafunzo ya muda mfupi, mrefu na wa kati kulingana na mahitaji yatakayowasilishwa na JKCI, kwa lengo la kubadilishana uzoefu pamoja na kuwapa mbinu mpya za matibabu hayo ya kisasa.

"Taasisi yetu inapokea wagonjwa tofauti kutoka nchi nyingi kama Marekani, Afrika na Asia pia. Tunatoa matibabu ya kibingwa, lakini hasa aina mpya ya upasuaji wa valvu ya mshipa mkubwa wa damu (Aortic Valve) bila kufungua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implantation procedure - TAVI).

"Tunafanya upasuaji pia wa kisasa kwa mishipa iliyoziba bila kufungua kifua, mgonjwa atakaa hospitalini kwa siku moja pekee, inayofuata ataruhusiwa, kuna tiba za aina tofauti ambazo zimekuwa za kisasa duniani," alisema Dk. Chandra.

Alisema, kutokana na huduma za matibabu bobezi na kibingwa zinazoendelea kutolewa JKCI, matarajio ni kuwa kwa miaka 10 ijayo taasisi hiyo itaweza kutekeleza upasuaji wa aina tofauti, Medanta itatoa mafunzo kwa wataalamu wa JKCI, yasiyopungua kipindi cha mwaka mmoja huko India.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo na Mkurugenzi wa Magonjwa ya Moyo JKCI, Dk. Tatizo Waane, alisema ujio wa bingwa huyo nchini, umelenga kuwajengea uwezo wanataaluma wa taasisi hiyo, wakiwamo madaktari.

"Siku ya jana Dk. Chandra, alipowasili jioni (juzi), alifanikiwa kufanya upasuaji wa moyo kupitia tundu ndogo kwa wagonjwa wawili, akishirikiana na timu ya JKCI, lakini leo (jana) tunafanya kwa wagonjwa watatu au wanne kabla hajaondoka," alisema Dk. Waane.

Alisema kwamba Medanta ni miongoni mwa taasisi zinazotoa matibabu ya kibingwa nchini India, ikiwa na utaalamu mkubwa na ikiahidi kushirikiana na JKCI hasa kuwajengea uwezo wataalamu wa tiba ya moyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ya fedha shuleni ndio mustakabali chanya kwa vijana

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikiendesha kampeni ya masuala jumuishi ya kifedha kwa makundi mbalimbali ili kupanua uelewa kuhusu masuala yanayohusu sekta hiyo.

Lengo la kuwapo kwa kampeni hiyo ni kuwawezesha Watanzania kuwa na uelewa kuhusu fursa zipatikanazo katika sekta ya fedha pamoja na kuepuka madhara yanayoweza kuwapata ikiwamo kuingia katika mikopo umiza.

Mbali na kuweka uelewa mpana kuhusu masuala ya fedha ikiwamo mikopo, kampeni hiyo pia inahusu kuwajengea uwezo wananchi kuwa na nidhamu ya matumizi sahihi ya fedha kupitia uwekezaji na utunzaji wa fedha katika taasisi zilizosajiliwa zikiwamo benki.

Aidha, serikali kwa kushirikiana na wadau hao, imekuwa ikitoa elimu kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu namna ya kutumia mifuko ya uwekezaji na masoko ya mitaji katika kununua hisa, hivyo kushiriki katika uchumi wa nchi na hatimaye kujijengea ukwasi kwa maisha yajayo hasa baada ya kuhitimu elimu. Kwa kufanya hivyo, watu wa makundi mbalimbali wamejengewa uwezo na uelewa kuhusu matumizi sahihi ya fedha kwa ajili ya maendeleo yao na vizazi vyao.

Hatua hiyo ya kutoa elimu ya fedha, imesisitizwa zaidi na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwamba ni muhimu sasa ikaanzia katika ngazi ya shule ili kuwaandaa vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Akizungumza juzi na washiriki wa mafunzo ya uongozi na usimamizi jumuishi na endelevu kwa wanawake yanayofanyika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kwamfipa wilayani Kibaha, Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa, alisema elimu ya fedha nchini iko chini.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni vyema elimu ikaanzia ngazi ya shule huku akisisitiza wazazi kushiriki kuwafundisha watoto kuweka akiba wakiwa wadogo. Alisema ili kufanikisha azma hiyo, serikali inaandaa sera itakayoyajumuisha makundi mbalimbali kuhusu masuala ya fedha, vijana wakiwa miongoni mwa walengwa.

Ni ukweli kwamba vijana wengi nchini, kutokana na ukosefu wa elimu ya fedha, wanakosa nidhamu pindi wanapopata fursa ya kupata nafasi za ajira. Vijana wengi mara wapatapo fedha, badala ya kuwekeza au kuzitumia kwa manufaa yao ya baadaye kwa kuwekeza au kufanya mambo ya maana, huishia kutumia kwa anasa ikiwamo ulevi. Matokeo yake, maisha yao huwa ya shida na taabu kwa sababu ya kukosa mwelekeo mzuri kimaisha hasa katika matumizi ya fedha.

Kutokana na ukweli huo, kama alivyosema aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa, Kanali Joseph Simbakalia (mstaafu), elimu kuhusu fedha inatakiwa kuenezwa kwa vijana kuanzia ngazi ya shule ili kuwaimarisha na kuwafanya kuwa imara. Simbakalia alisisitiza kwamba makuzi bora kwa vijana tangu wakiwa wadogo ndio msingi imara wa kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha.


Kauli ya kiongozi huyo ambaye ni mmoja wa wasomi na hazina kwa taifa, ni sawa na kauli kwamba nyumba bora ambayo chanzo chake ni msingi imara. Msingi mbovu husababisha kuwapo kwa nyumba mbovu, kadhalika nyumba imara chanzo chake ni msingi imara.

Ni wazi kwamba elimu ya fedha ikitolewa kuanzia ngazi ya shule itasababisha vijana wengi kuwa na uelewa kuhusu matumizi bora ya rasilimali hiyo kwa sababu watakapokuwa wakubwa na kuanza kufanya kazi au biashara, watapata nafasi ya kutumia kwa umakini ikiwamo kuwekeza katika masoko na mifuko ya fedha na dhamana.

Mfano hali ni katika familia za watu wa asili ya Kiasia ambao wengi ni wafanyabiashara, wazazi huanza kuwafundisha masuala ya fedha ikiwamo nidhamu katika matumizi wakilenga kuwafunza namna bora ya kupata mafanikio katika shughuli watakazofanya watakapoanza kujitegemea au kurithi biashara walizozikuta.

Kama wahenga wasemavyo samaki mkunje angali mbichi, suala la kutoa elimu ya fedha kwa vijana kuanzia shuleni ni mwafaka na linapaswa kuungwa mkono. Serikali inapaswa kuandaa sera ya mafunzo hayo na kuanza kutumika mapema kwa mustakabali wa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# HESLB ikumbuke kozi stashahada

**NI** takribani mwaka mmoja sasa, tangu serikali ilipotangaza vipaumbele vipya kwenye elimu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada.

Vipaumbele hivyo vimejikita katika maeneo sita ambayo yalitengewa Sh. bilioni 48 kuwakopesha wanafunzi 8,000 waliokuwa wafanyiwe udahili katika mwaka wa masomo 2023/24.

Mwaka wa masomo mpya wa 2024/25 unaanza na waombaji wanatarajia kuanza masomo wiki ijayo, na huu ndiyo wakati wa kuwakumbuka Watanzania hasa vijana wanaojikita katika taaluma tofauti zinazohusika na kozi za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, Oktoba mwaka jana, anazindua 'Mwongozo wa Utoaji Mikopo ya Elimu kwa Wanafunzi wa Stashahada' kwenye ofisi ndogo za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dar es Salaam.

Anasema uamuzi huo ni marekebisho ya sheria ya HESLB ya mwaka 2017 wa kuwahusisha wanafunzi wa ngazi hiyo.

Aidha, anasema ni mara ya kwanza kwa Tanzania kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada.

Kwa maendeleo ya taaluma ni hatua njema. Lakini, ikumbukwe huo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutaka wanafunzi wa vyuo vya kati kunufaika na mikopo ya serikali.

Anasema kinachofanyika ni utekelezaji wa maazimio ya Afrika kuhusu kuendeleza rasilimali watu.

Mikopo hiyo ipo katika vipaumbele sita na mahsusi kwa wanaosoma kozi za afya na sayansi shirikishi; elimu, zipo stashahada za ualimu wa fizikia, hisabati na amali.

Kadhalika kuna usafiri na usafirishaji, uhandisi wa nishati, madini na sayansi ya ardhi, kilimo na mifugo.

Mbali na vipaumbele hivyo, ni wazi serikali imesahau eneo muhimu kulipatia mikopo nalo ni stashahada ya TEHAMA ambayo ndio msingi na tegemeo kubwa kwenye sekta zote za maendeleo kuanzia afya, kilimo, mifugo, fedha, maji, elimu, nishati na madini.

Hivi sasa ubunifu na uandaaji wa shughuli za maendeleo unawategemea wataalamu wa TEHAMA ambao ndiyo wabobezi wa mifumo na mbinu tofauti na kutoa tafsiri za mambo ya kufanya na jinsi ya kuyafanikisha kielektroniki.

Kadhalika, katika sekta ya afya kipaumbele kimojawapo cha kupatiwa mkopo huo, asilimia karibu 70 ya kazi zake zinafanyika kwa kutegemea teknolojia.

Ni kazi zote za matibabu kwenye hospitali kuu na kwenye vituo vya afya ambako, wanahitajika wataalamu wa TEHAMA kama ilivyo viwandani na kwenye usafirishaji.

Vifaa vilivyoko hospitalini vingi ni vya kidijitali kuanzia X-ray, CT Scan, MRI, Ultra sound na hata vipimo vidogo enzi za kutumia muda mrefu kusubiri majibu ya vipimo kwa magonjwa maabara umepitwa na wakati, kutokana na kukua kwa teknolojia.

Kadhalika, hivi sasa uandikishaji wa wagonjwa kuanzia ngazi ya chini hadi rufani, hutegemea TEHAMA na si ile mfumo wa majalada uliokuwa unapoteza taarifa kwa vile kila wakati mafaili yalinyofoka leo kila kitu kinatunza mtandaoni.

Kadhalika taarifa zinamfikia daktari kupitia kompyuta ofisini kwake moja kwa moja linapokuja suala la mgonjwa fulani anayemhudumia.

Matibabu hutumia tiba mtandao, kuna aina kadhaa za upasuaji na upangaji wa dawa kwa wafamasia wakitegemea teknolojia ya kompyuta kwa kutunza kumbukumbu kujua iwapo dawa fulani ipo stoo au la, na inaweza kupatikana wapi, si kama awali ilihitaji mtu azame stoo kupekua, ndipo ajue idadi ya dawa zilizopo.

Madaktari bingwa miaka hii wanabadilishana uzoefu na wenzao walioko nje na ndani ya nchi kwa njia ya TEHAMA wakiunganisha mawasiliano ya video na wenzao popote duniani, kumfanyia upasuaji mgonjwa bila kuhitaji kumsafirisha au bingwa kusafiri na kumfikia kwa huduma.

Hebu fikiria, hivi sasa kwa kutumia programu tumishi (application), mtandaoni huduma ya M-mama, imeleta faraja miongoni mwa wajawazito na wazazi kwa kuokoa mamia ya wanawake na vifo vyao kupungua.

## Waziri ataja sababu watumishi kushinda rufani wanapofukuzwa

**Na Lusungu Helela,** DODOMA

UKOSEFU wa weledi katika kushughulikia mashtaka ya kinidhamu kwa watumishi wa umma ni chanzo cha serikali kuingia gharama pindi mtumishi anapokata rufani dhidi ya hatua iliyochukuliwa dhidi yake ikiwamo kuachishwa kazi.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amesisitiza kuwapo na weledi katika kushughulikia masuala ya kinidhamu.

Sangu alisema hayo jana jijini hapa baada ya kushuhudia usikilizaji wa rufani na malalamiko ya baadhi ya watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliofanywa na mamlaka za ajira na nidhamu katika maeneo yao ya kazi wakitoa utetezi wao mbele ya Makamishna wa Tume.

Alisema mamlaka hizo zimekuwa hazitoi fursa ya kujitetea kwa mtumishi anayetuhumiwa na kosa fulani kabla ya kuhukumiwa jambo ambalo ni moja ya misingi ya utoaji haki kwa mujibu wa Katiba ya nchi na sheria zilizoko.

Kamati za uchunguzi zinazoundwa, alisema zinapaswa kutekeleza wajibu wao ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taarifa zao za uchunguzi kubainisha iwapo makosa waliyoshtakiwa nayo watumishi watuhumiwa yamethibitika au kutokuthibitika kutendeka.

Alisema kukosekana kwa mambo hayo, kumekuwa kukiiumiza serikali kwa kulazimika kulipa mshahara mtumishi katika kipindi chote alichokuwa amefukuzwa kazi au kusimamishwa.

Mbali na gharama hizo ambazo serikali hulazimika kuingia, pia alisema katika hatua za mwanzo pindi mtumishi anapotuhumiwa kuwa na makosa huanza mchakato wa kuunda kamati za uchunguzi, wajumbe wake hulipwa posho ambayo ni fedha za serikali.

Kutokana na hali hiyo, Sangu alisema anatamani kuona rufani na malalamiko yanayopelekwa Tume ya Utumishi wa Umma yanamalizika katika ngazi ya chini yakiwa yamefanyika kwa weledi na idadi kupungua ili tume hiyo ijikite kwenye masuala ya ukaguzi na mafunzo ili kuboresha ufanisi katika utumishi wa umma.

Alisema mashtaka mengi yanayopelekwa katika tume hiyo yamebainika kuwa na kasoro za wazi, hivyo kumpa nguvu mtumishi mtuhumiwa kuwasilisha rufani na malalamiko yake katika Tume ya Utumishi wa Umma.

**Alisema mamlaka hizo zimekuwa hazitoi fursa ya kujitetea kwa mtumishi anayetuhumiwa na kosa fulani kabla ya kuhukumiwa jambo ambalo ni moja ya misingi ya utoaji haki kwa mujibu wa Katiba ya nchi na sheria zilizoko.**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian (wa pili kushoto), akizindua kituo cha Taarifa za Utalii, wakati wa Tamasha la Utalii la Usambara 2024, katika viwanja vya Nyerere Square, wilayani Lushoto, mkoani Tanga mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Zephania Sumaye. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Kortini madai kutumia jina la JK kutapeli

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mabwepande, Shembiu Shekilaghe (38), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya Kinondoni, Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka ya kutoa taarifa za uongo na kujiwasilisha kama Jakaya Mrisho Kikwete huku akijua si kweli.

Wakili wa Serikali, Salma Jafari, akisoma mashtaka hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Hawa Magesa, alidai mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka 14 huku mashtaka ya kwanza, ya pili na tatu yakiwa kutoa taarifa za uongo.

Ilidaiwa kuwa Septemba 2, mwaka huu, mshtakiwa akiwa katika eneo lisilojulikana ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa taarifa za uongo kupitia akaunti ya mtandao wa kijamii ya Facebook yenye jila la Mrisho Jakaya Kikwete akisema: "Ukiweka akiba ya 49,000 utapata mkopo wa 300,000 na marejesho ni Sh. 30,000 kila mwezi kwa muda wa miezi 10."

Katika tarehe hiyo, ilidaiwa kuwa kupitia akaunti hiyo pia alitoa taarifa akisema: "Ukiweka akiba ya 59,000 utapata mkopo wa Sh. 400,000 marejesho ni Sh. 40,000 kila mwezi kwa muda wa miezi 10."

Pia kupitia akaunti hiyo, alidaiwa kutoa taarifa kuwa: "Ukiweka akiba ya Sh. 69,000 utapata mkopo wa 500,000 marejesho ni Sh. 50,000 kila mwezi kwa miezi 10."

Ilidaiwa Juni 7, mwaka huu, katika eneo la Kigamboni, Dar es Salaam, kupitia mtandao wa kijamii wa Facebook, mshtakiwa kwa nia ovu alijiwasilisha kama Mama Salma Kikwete, mke wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne.

Pia tarehe hiyo na kupitia akaunti iliyosajiliwa kwa jina la Salma Foundation, ilidaiwa mshtakiwa alitoa taarifa za uongo akisema: "Ukiweka akiba Sh.105,000 utapata mkopo wa Sh. milioni moja, marejesho Sh. 100,000 kila mwezi kwa miezi 10 na ukiweka Sh. 205,000 utapata mkopo wa Sh. milioni mbili marejesho Sh. 200,000 kila mwezi kwa miezi 10."

Mashtaka matano ni ya kutumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina la mtu mwingine huku ikidaiwa kuwa Septemba 3, mwaka huu, katika eneo la Mji Mpya, Mabwepande, mkoani Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akitumia namba ya simu iliyosajiliwa kwa majina ya Matias Ngowi, Modesta Marumi, Jane Mhanga, James Zephania na Amini Omary.

Mashtaka mengine ni ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu ikidaiwa kuwa Julai 31, mwaka huu, kupitia namba iliyosajiliwa kwa jina la Tatu Sunzula, mshtakiwa alijipatia fedha Sh. 49,000 kutoka kwa Albert Athanas kwa kudai atampa mkopo wa Sh. 500,000 huku akijua si kweli.

Pia Agosti 17, mwaka huu, kupitia namba hiyo hiyo, anadaiwa alijipatia Sh. 100,000 kutoka kwa Samson Mwandawila kwa kudai atampatia mkopo wa Sh. 800,000 huku akijua si kweli.

Mshtakiwa pia anadaiwa kuwa Agosti 9, mwaka huu, kupitia namba hiyo, alijipatia Sh. 100,000 kutoka kwa Rudi Maduka akidai atampatia mkopo wa Sh. 1,000,000 kupitia taasisi yake ya Jakaya Kikwete Foundation.

Baada ya kusomewa mashtaka dhidi yake, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo.

Jafari alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, hivyo aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kusoma hoja za awali.

Hakimu Magesa aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 10, mwaka huu, kwa ajili ya kusomwa hoja za awali. Mshtakiwa huyo alirudishwa rumande baada ya kukosa wadhamini.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Katambi aagiza halmashauri kuwezesha vijana

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

NAIBU Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, ameziagiza halmashauri nchini kutekeleza maagizo ya kuwawezesha vijana ikiwamo kuwapatia mikopo ili kujiendeleza kiuchumi kupitia sekta ya kilimo.

Akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi zana za kilimo kwa vijana 50 wa Manispaa ya Iringa, Katambi alisema serikali imeendelea kuweka mikakati madhubuti ya kisera ikiwamo Sera ya Elimu ya Mwaka 2007 na Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 ambayo imefanyiwa maboresho mwaka 2024 ambayo inasaidia kuratibu masuala ya maendeleo ya vijana.

Katambi alisema serikali inatambua uwapo wa wadau muhimu ambao wamekuwa na mchango mkubwa kwa serikali kuchangia shughuli za maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi wakiwamo wanawake kupitia Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID).

"Tunawashukuru kwa sababu wamekuwa washiriki wakubwa katika kuisaidia serikali kufika azma yake ya kisera, kisheria na katika mipango ambayo tumeiweka kuhakikisha tunaleta ustawi kwa vijana lakini makundi maalumu yakiwamo ya watu wenye ulemavu kiuchumi," alisema Katambi.

Kuhusu utoaji wa vifaa vya kilimo, alisema licha ya serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kama USAID kupitia mradi wa Feed the Future Tanzania Imarisha Sekta Binafsi (PSSP), halmashauri zina wajibu wa kuhakikisha vijana wanawezeshwa ili kuzalisha na kujiajiri kupitia kilimo.

"Natambua kwamba TWCC imeendelea na mradi wa Feed The Future Imarisha Sekta Binafsi na mpo katika mikoa mbalimbali nchini lakini kwa mkoa wa Iringa kazi hii mlianza kuifanya tangu mwaka 2003 mkishirikiana na serikali ya mkoa na halmashauri katika kuongeza mnyororo wa thamani kwenye sekta ya kilimo katika kuwekeza fedha.

"Fursa hii inafungua fursa za kiuchumi kwa vijana, hivyo nizitake halmashauri kuwashika mkono vijana hawa ili kuzalisha kupitia shughuli za kilimo," alisema.

Rais wa TWCC), Mercy Silla, alieleza walivyofanikiwa kuwaunganisha vijana kupitia mradi huo akibainisha kuwa kupitia mradi huo, zaidi ya ajira 80 zimezalishwa katika mkoa wa Iringa huku zaidi ya vijana 300 wakirasimisha biashara zao ambazo zimewafungulia fursa zingine kupitia taasisi za fedha.

Pia alisema TWCC imewasaidia vijana kupata mitaji ya biashara kupitia benki na taasisi za fedha pamoja na kuendelea kuimarisha vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA) jambo ambalo limewasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja ambacho tumefanya kazi kupitia malengo tuliojiwekea, tumefanikiwa kuwafanya vijana waendelee kusalia katika mradi tofauti. Awali, tuliambiwa vijana hawawezi kufanya kazi za kilimo lakini vijana wa Iringa wamekuwa mfano katika kutekeleza majukumu ya mradi," alisema Silla.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Maendeleo ya Ubalozi wa Marekeni nchini Tanzania, Erick Jonson, mradi wa Feed the Future Tanzania ni sehemu ya juhudi za kimataifa za kudhibiti njaa na kuhakikisha usalama wa chakula, ukilenga hasa wakulima wadogo, hususan wanawake.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwanda, alisema kupitia mapato ya ndani, halmashauri imetenga Sh. milioni 900 kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 ambayo inagawanyika kwa asilimia nne kwa wanawake, nne kwa vijana na mbili kwa wenye ulemavu. Alisema fedha hizo zitaanza kutolewa baada ya maelekezo ya serikali.



Mtaalamu wa mafunzo ya huduma ya kwanza kutoka Chama cha Msalaba Mwekundu, Peter Bongo, akitoa maelezo ya jinsi ya kumhudumia mtu aliyepata ajali, wakati wa uzinduzi wa mpango wa kutoa elimu na mafunzo kwa madereva wa bodaboda wa mkoa wa Dar es Salaam, Mikocheni jana. Mpango huo unatekelezwa na chama hicho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwamo Jeshi la Polisi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TAMWA yatangaza kampeni mazingira kuwezesha wanafunzi kubaki shuleni

**Na Beatrice Moses**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimepaza sauti kuhamasisha wadau wa elimu na jamii kwa ujumla kushughulikia mizizi ya watoto kuacha shule kwa kuunda mazingira yanayowezesha wanafunzi kubaki shuleni, kusaidia watoto walio katika mazingira magumu, hasa wasichana na wenye ulemavu.

Katika kufanya hivyo, TAMWA imetangaza kufanya kampeni ya mwezi mzima inayolenga kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwapeleka watoto shuleni kwa wakati, hasa wale walio hatarini zaidi kuacha shule.

Meneja Miradi na Mikakati wa TAMWA, Sylvia Daulinge, alisema hayo juzi Dar es Salaam wakati akizungumzia kuhusu uzinduzi wa makala mpya inayoangazia elimu bora na elimu jumuishi kwa wanafunzi katika shule za umma ikiwa sehemu ya kutekeleza kampeni hiyo.

Daulinge alisema makala hiyo ya video inatoa uchambuzi wa kina kuhusu changamoto zinazoyakumba makundi yaliyotengwa kama vile wasichana, watoto wenye ulemavu na wanaotoka familia maskini kuhamasisha upatikanaji wa elimu bora na jumuishi kwa watoto.

"Makala imeleta pamoja sauti za watoto, wazazi, walimu, mashirika ya kiraia (CSO) na ofisa wa serikali, ikianzisha mazungumzo kuhusu jinsi ya kuvunja vikwazo vinavyowazuia watoto kupata elimu bora na si bora elimu. Pia inasisitiza haja ya haraka ya kukabiliana na changamoto hizi kupitia uwezeshaji wa jamii, ushirikiano na watu wenye ushawishi, na kuboresha sera za elimu nchini," alisema.

Kampeni hiyo ambayo inalenga kuzunguza na walimu 200, inafanywa na TAMWA kwa kushirikiana na shirika la kimataifa lisilo la kiserikali - We World ambalo limesaidia mradi wa Pamoja Tudumishe Elimu.

Alisema ushirikiano wa pamoja utasaidia kuhakikisha uwakilishi mzuri wa changamoto za kipekee zinazowakumba watoto katika mazingira mbalimbali, na utofauti huo unatoa taswira ya kina na pana ya hali ya elimu nchini ambayo itasaidia kubadilika kwa mazingira ya ufundishaji na uandikishwaji wa watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alikaririwa akisema kila mtoto anastahili elimu bora, elimu jumuishi na yenye usawa, sio tu kuhusu mustakabali wao, bali ni mustakabali wa jamii nzima.

"Watoto wanaacha shule hasa katika maeneo yenye uhaba wa huduma hii inatokana na umaskini, umbali mrefu wa shule, mila na desturi za kijamii zetu na ukosefu wa rasilimali za kutosha za kumuwezesha mtoto kwenda shuleni," alisema.

Katika kuhakikisha elimu bora, jumuishi na yenye usawa kwa kila mtoto ni uwekezaji muhimu katika mustakabali wa taifa.

# Ataka elimu ya fedha kuanzia shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, amesema elimu ya fedha ni muhimu kuanzia shuleni ili kuwaandaa vijana kushiriki shughuli za kiuchumi.

Amesema elimu ya fedha bado iko chini Tanzania na kuwataka wazazi kushiriki kuwafundisha watoto kuweka akiba wakiwa bado wadogo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na washiriki wa mafunzo ya uongozi na usimamizi jumuishi na endelevu kwa wanawake yanayofanyika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kwamfipa Kibaha.

Alisema serikali inatengeneza sera kuhakikisha Watanzania wanashiriki kiuchumi na kwamba elimu ya fedha ikianza kufundishwa mapema kwa watoto shuleni itasaidia kuleta mabadiliko yanayolengwa.

Alisema serikali imeendelea kufikisha huduma muhimu kwa wananchi ikiwamo umeme, maji na barabara, lengo likiwa ni kuwainua kiuchumi kwa kuwapa fursa za kushiriki katika uzalishaji bila vikwazo.

Alikumbusha wananchi kuchagua viongozi bora kwenye uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa watakaowavusha kimaendeleo huku akisisitiza wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea.

Beng'i alisema wanawake ni kati ya kundi linalojiamini kwa kutumikia mambo mengi kwa wakati mmoja na wanatakiwa kugombea nafasi za uongozi kuendelea kuonesha umahiri wao wa kufanya shughuli za malezi na kuongoza kwenye jamii.

Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, akiwa katika mafunzo hayo alisema katika jamii, wawezeshaji wakubwa ni wanawake na hiyo imetokana na malezi wanayoyapata wakiwa bado wadogo na kwamba mafunzo hayo yatazidi kuwaimarisha na kuwafanya kuwa imara.

Meneja idara ya mafunzo na ustawi kutoka shule hiyo, Kabula Igambwa, alisema mafunzo yatasaidia kuongezeka kwa utambuzi kwa wanawake viongozi, kuwa na uongozi shirikishi na wenye ushindani.



## CCM yatoa maagizo usimamizi fedha za maendeleo

**Na Mary Mosha,** SAME

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro imewataka watumishi katika idara ya afya kuongeza umakini katika usimamizi wa fedha zinazoletwa na serikali kwa ajili ya maendeleo.

Kauli hiyo imetolewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) kupitia Mkoa wa Kilimanjaro, Seleman Mfinanga wakati wa ukaguzi wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa wajumbe wa kamati hiyo wilayani Same.

Mjumbe huyo akiongozana na jopo lake alitembelea mradi wa uboreshaji wa Kituo cha Afya Hedaru unaogharimu Sh. milioni 728 pamoja na mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Suji Malindi ambapo unagharimu Sh. milioni 470.26.

Mfinanga alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma zinasogea kwa wananchi na kuwataka watumishi wa umma kuhakikisha lengo la Rais Samia linatimia kwa vitendo.

Katika hatua nyingine kiongozi huyo aliwataka watumishi kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi kwa vitendo na kufuata kanuni zinazowaongoza katika kazi.

Aidha, aliwataka kuhakikisha fedha zinapoletwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitumike kwa wakati na kuzingatia pia thamani ya fedha ili wananchi wanufaike na fedha za serikali.

Akisoma taarifa ya uboreshaji Kituo cha Afya Hedaru, Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Benethson Rutahindurwa, alisema mradi huo umeibuliwa kwa lengo la kuboresha na kuongeza upatikanaji wa huduma ya afya hususani za upasuaji, kuhifadhi miili na kutoa huduma ya X-ray.

Alisema kituo hicho cha afya kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi wakiwamo mtaalamu wa mionzi na daktari anayefanya upasuaji kwa sasa ni mmoja pamoja na wauguzi.

Aidha, alisema kuwa kukamilika kwa jengo la mionzi kutaondoa adha kwa wananchi zaidi ya 40,630 ambao wanatembea zaidi ya kilomita 50 kwa ajili ya kupata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Same.

# Wilaya 106 zaunganishwa na mkongo wa taifa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL), limesema kati ya wilaya 139 zilizoko Tanzania Bara hadi sasa tayari wamefanikiwa kuunganisha wilaya 106 katika mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Ufundi na Uendelezaji kutoka TTCL, Cecil Francis, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye kongamano la Connect 2 Connect.

Kongamano hilo limefunguliwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa na limewakutanisha wadau wa mawasiliano wa ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema kwa wilaya 33 ambazo bado hazijafikiwa na mkongo wa taifa wa mawasiliano mwaka huu wa fedha serikali imeshatenga bajeti ya kwenda kukamilisha shughuli hiyo, ili kuhakikisha wilaya zote zinaunganishwa.

Alisema mkongo wa mawasiliano wa taifa ni kiungo kikuu cha mawasiliano ya sauti na Intaneti ambapo inaunganishwa na mikongo ya baharini ambayo inaleta intaneti nchini.

"Mkongo wetu wa taifa wa mawasiliano ni kiungo kikuu cha mawasiliano ya sauti, lakini vilevile na intaneti na tunaunganisha na mikongo ya baharini ambayo inatuletea intaneti hapa nchini na sisi pia tunaunganisha na nchi za jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi," alisema.

Pia alisema shirika hilo linaendelea kuboresha maunganisho ya mkongo wa kusogeza kwenye vituo vya baharini vilivyoko Mombasa nchini Kenya.

Alisema: "Kazi kubwa tuliyonayo TTCL, ni kuhakikisha tunatoa mchango wa mawasiliano kwa mkongo tunayojenga inafika kila sehemu ikiwa na ubora wa hali ya juu kwa ajili ya kufikisha huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za matumizi".

Alisema shirika hilo kupitia mkongo wa taifa wa mawasiliano wamefanya kazi ya kuunganishwa kwa mawasiliano mikoa kwa mikoa na wilaya kwa wilaya.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Helios Towers, Gwakisa Stadi, alisema kampuni hiyo kwa hapa nchini inasimamia minara zaidi ya 400 na wana wateja zaidi ya 10,000.

Alisema kazi kubwa ya minara hiyo ni kuunganisha huduma za mawasiliano na wateja wao wakubwa ni kampuni ya simu, kampuni za usambazaji wa inteneti na televisheni zilizoweka vifaa vyao vya mawasiliano kwenye minara hiyo.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Muheza, Hamis Mwinjuma (kushoto), akikabidhi cheti cha pongezi kwa Polisi Kata ya Kwafungo, Mkaguzi Msaidizi Novatus Malima, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi, kutokana na jitihada za jeshi hilo katika kupambana na kuzuia vitendo vya kiuharifu kupitia mradi wa Polisi Jamii. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wagombea Kata ya Pasua kubeba agenda ukosefu huduma za afya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAWAKE na vijana walioonyesha nia ya kugombea nafasi za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wamesema wako tayari kubeba changamoto ya huduma za afya katika Kata ya Pasua, Manispaa ya Moshi kama ajenda kuu ya uchaguzi huo.

Akizungumza jana katika kikao cha wadau wa mradi wa 'Sauti ya Haki', Abdalah Massawe alisema kutokana na huduma za afya kutopatikana kwa uhakika, ajenda yao kuu ya kutaka kuchaguliwa ili kuwaongoza wananchi ni kuzungumzia utatuzi wake.

"Kwa mfano, Pasua changamoto kubwa ni huduma za afya, ambapo wananchi hawapati huduma kwa wakati na waathirika ni wazee, wajawazito na watoto. Maana yake, tunatakiwa sasa tubebe jukumu la kuwasiliana na wahusika wanaosimamia afya katika ngazi ya halmashauri ili kuhakikisha hiyo changamoto inafanyiwa kazi na kutatuliwa," alisema.

Mradi huo wa miezi sita, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT), unalenga kuendeleza majukwaa ya wanawake kwa ajili ya haki za uongozi kuelekea uchaguzi huo.

Veronica Alex, mkazi wa Pasua, alisema ajenda nyingine watakayoibeba ni ubovu wa barabara za Pasua, kwa kuwa nyingi ni mbovu na hazipitiki kirahisi.


Ofisa Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa wa Shirika hilo, Peter Mashingia, aliwataka wanawake na vijana wenye nia ya kugombea katika uchaguzi huo kutambua wajibu huo kwa sababu mwakilishi wa wananchi ambaye ni kiongozi wa kisiasa, anabeba hatima ya watu wake kwa miaka yote atakayokuwa madarakani.

"Unapotaka kugombea hizi nafasi, hebu waza utatengenezaje mifumo ya kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji wa fursa mtawalia, ili vijana na wanawake waweze kunufaika na hizo fursa; kwa ajili ya kuchakata au kushiriki katika mchakato wote wa uzalishaji na matumizi sahihi ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo, kujiimarisha na kuongeza kipato halali," alisema.

Mratibu wa mradi huo, Veronica Ollomi, alisema pamoja na uchaguzi mradi huo utashughulikia uimarishaji haki za kifeminia na haki za kijamii.

Kwa mujibu wa Ollomi, kata zilizolengwa kujengewa uwezo ni Pasua na Ngangamfumuni (Manispaa ya Moshi), na Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi).

Zaidi aliongeza: "Na hata tulivyotoa taarifa kwa Mtendaji wa Kata na waliohusika kuwaita tuliwaambia kwamba sifa ya kwanza au kigezo cha kwanza, awe ana nia ya kutamani kushiriki kwenye mchakato wa kugombea nafasi za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa".



# Shule yakosa umeme, yapeleka kilio chake kwa mbunge

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

SHULE ya Sekondari Mwamashele wilayani Shinyanga imeomba kupatiwa huduma ya umeme, ili kupunguza gharama za uchapishaji wa mitihani pamoja na wanafunzi waweze kujisomea nyakati za usiku.

Ombi hilo limetolewa juzi na Mkuu wa Shule hiyo, Denis Fungo, shuleni hapo kwa Mbunge wa Kishapu, Boniface Butondo aliyefanya ziara ya ukaguzi wa majengo.

Fungo alisema kuwa ukosefu wa huduma hiyo kunasababisha shule hiyo kutumia gharama kubwa kuchapisha mitihani.

Alisema wanatumia zaidi ya Sh. 700,000 kuchapisha mitihani lakini fedha za serikali ambazo wanazipokea kila mwezi za elimu bila malipo ni Sh.300,000 ambayo haitoshi kumaliza kazi hiyo.

"Shuleni hapa tumeshafanya "wirering" tunasubiri kuvutiwa umeme tu, ili tupunguze gharama za uchapishaji mitihani," alisema Fungo.

Akizungumza shuleni hapo alipoitembelea kuangalia maendeleo yake ukiwamo na ujenzi wa bweni la wasichana, Butondo aliahidi kufanya jitihada zote kwamba hadi kufikia Oktoba umeme shuleni hapo uwe umeshawaka na kuondoa gharama hizo kubwa za uchapishaji mitihani.

**Ombi hilo limetolewa juzi na Mkuu wa Shule hiyo, Denis Fungo, shuleni hapo kwa Mbunge wa Kishapu, Boniface Butondo aliyefanya ziara ya ukaguzi wa majengo.**

"Umeme ukifika hapa shuleni utakuwa na faida kubwa sana sababu mtakuwa na mashine ya kuchapisha mitihani na mtachapisha hapa hapa shuleni yakiwamo majaribio, na hakuna tena kwenda Mhunze kuichapisha kwenye "stationary" za watu binafsi na kutumia gharama nyingi," alisema Butondo.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Kishapu, Elias Turnbull, alipopigiwa simu na mbunge huyo kueleza ni lini atapeleka huduma ya alisema kutokana na bajeti kuwapo ya shule hiyo, kwamba haitapita Oktoba umeme utawashwa shuleni hapo.

Baadhi ya wanafunzi shuleni hapo walisema huduma ya umeme ni muhimu kwa sababu watakuwa na muda mwingi wa kufanya mazoezi ya majaribio yaliyochapishwa pamoja na kupata muda mwingi wa kujisomea.



Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Boniphace Butondo, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwamashele, alipofanya ziara shuleni hapo, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Bil.12/- kuboresha barabara Tabora

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA) mkoani Tabora umesaini mikataba 27 ya awamu ya kwanza yenye thamani ya Sh.bilioni 12.2 kwa makandarasi 22.

Lengo la mikataba hiyo ni kufanya matengenezo na maboresho ya mtandao wa barabara katika halmashauri saba mkoani hapa.

Akizungumza juzi wakati wa utiaji saini wa mikataba hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, aliwaonya makandarasi watakaotekeleza miradi hiyo kutokufanya udanganyifu katika hati mbalimbali na uchelewaji wa miradi hiyo.

"Sitakuwa mvumilivu kwa mkandarasi ambaye kwa namna yoyote ile atafanya udanganyifu katika hati mbalimbali na uchelewaji wa ukamilishaji wa matengenezo ya barabara hizo," alisema Chacha.

Aidha, aliwataka wananchi kuhakikisha wanatunza miundombinu ya barabara hizo na kutokuwa sehemu ya watu wanaofanya uharibifu wa miradi hiyo inayogharimu fedha nyingi za serikali.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Tabora, Lusako Kilembe, alisema kwa mwaka 2024/25 wametengewa Sh.bilioni 25.09 kama sehemu ya bajeti ya matengenezo na ukarabati wa barabara kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya bajeti.

Kilembe alisema kati ya fedha hizo Sh.bilioni 12.2 zitatumika kwenye ujenzi na ukarabati wa mtandao wa barabara, ukihusisha ujenzi wa makaravati, uwekaji wa taa barabarani na ukarabati wa barabara kwenye halmashauri zote saba za mkoa huo.

"Lengo ni kuhakikisha mikataba yote itakayosainiwa inakwenda kuanza utekelezaji wa kazi hizi haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu zilizowekwa," alisema Kilembe.

# Wachimbaji madini watakiwa kuwania uongozi S/mitaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha Wachimbaji Wadogo wa Madini mkoani Shinyanga (SHIREMA) kimewataka wachimbaji hao kuhakikisha wanagombea nyadhifa mbalimbali katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Kimesema lengo ni kuwa sehemu ya kutoa maamuzi yatakayowasaidia kuondokana na utiriri wa kodi migodini.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hamza Tandiko, alibainisha hayo juzi wakati wa uchaguzi wa viongozi wa chama hicho mkoa wa kimadini Kahama, uliosimamiwa na Ofisa Madini Mkazi, Winfrida Mrema, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita.

Alisema kila mchimbaji madini mwenye sifa anatakiwa kugombea nafasi za uongozi wa serikali za vijiji, vitongoji, mitaa ili kupata wajumbe watakaokuwa washiriki katika vikao vya maamzi vya kupanga ushuru kwenye maeneo ya uchimbaji.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia kuondokana na malalamiko ya utiriri wa kodi kwa kuwa watakuwa na wawakilishi wa kuwasemea.

Tandiko alisema kwenye nafasi ya udiwani na ubunge wanao wawakilishi ambao wamekuwa wakiwasemea matatizo yao ngazi ya wilaya ya taifa na sasa na muda wa kupata viongozi ngazi za vitongoji na vijiji ambako ndipo uzalishaji unapofanyika.

"Migodi yetu ipo vijijini ambapo tunahitaji kupata viongozi kwenye uchaguzi huu wa serikali za mitaa, watakuwa wanatuwakilisha ngazi za halmashauri katika kutunga sheria na sera za ukusanyaji wa mapato na pale zitakapokuwa juu watakuwa na uwezo wa kujenga hoja na zikashuka, uzalishaji ukaongezeka na serikali ikapata kodi," alisema Tandiko.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa kimadini Kahama, Winfrida Mrema, alisema hatua ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura umeshafanyika.

Alisema hivyo ni wajibu wa wenye sifa kuchangamkia fursa hiyo ili kupata viongozi ngazi za vijiji na vitangoji ambao watashirikiana pamoja katika kutatua kero zinazowakabili wachimbaji.

Alisema serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uchimbaji kwa kutoa maeneo yenye madini ili kuondokana na uchimbaji wa kuhamahama kama ilivyokuwa hapo awali, wachimbaji kutumia nguvu nyingi kwenye uzalishaji lakini wanapata dhahabu ndogo, hali iliyokuwa ikiwafanya kushindwa kulipa mirabaha kwa kutorosha madini.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alisema Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, ameendelea kufuta leseni kubwa ambazo hazikuendelezwa kwa muda mrefu na sasa zinakwenda kutolewa katika makundi maalumu ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha kila mmoja ananufaika na uwepo wa rasilimali hiyo.

Alisema serikali imeleta wataalam wa utafiti wa maeneo yenye madini kutoka Chuo Kikuu cha Marekani ambao watawafundisha wataalamu wetu ili kupata ujuzi wa kutafiti maeneo hayo kwa kina.

Mhita aliwataka kuacha kujihusisha kwenye vitendo vya utoroshaji wa madini ambavyo vinasababisha serikali kuendelea kukosa mapato, kwamba wanaobainika wamekuwa wakichukuliwa hatua ikiwamo kuwafungulia kesi za uhujumu uchumi.



Ukurasa 12

**Ziara ACT-Wazalendo mikoani inavyoibua madudu mapya**



Ukurasa 13

Ndivyo madini ya kipekee yalivyo na nafasi kuipeleka nchi mbali



Ukurasa 14

**Mgogoro Israel Vs Hamas kuelekea kumaliza mwaka**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 25, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


KUTOKA JICHO LA WACHAMBUZI

# CHADEMA na Polisi kutunishiana misuli

**Na Mwandishi Wetu**



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe akiwa chini ya ulinzi wa polisi, alipokamatwa eneo la Magomeni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Jeshi la Polisi wameanza wiki kwa kutunishiana misuli baada ya serikali kupiga marufuku maandamano ya chama hicho, lakini viongozi wake wakaendelea kuhamasisha wanachama waandamane.

Vuta ni kuvute hiyo, inasababisha viongozi wa juu wa chama hicho kukamatwa, akiwamo Mwenyekiti Taifa Freeman Mbowe na Makamu Tundu Lissu, lakini baadaye wakaachiwa. Tukio hilo linalotokea jijini Dar es Salaam juzi, na baadhi ya wachambuzi wa siasa wanalizungumzia sakata hilo wakisema katiba inaruhusu lakini mazingira hayakuwa rafiki.

"Maandamano ya amani ni haki ya kikatiba ya kuelezea hisia zao, lakini hali ingekuwa tofauti kulingana na mazingira yaliyopo sasa," anasema Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya.

Anafafanua kuwa hatua zinazochukuliwa na polisi kuzuia maandamano hayo ni muhimu kwa wakati huu.

Ngawaiya ambaye ni kada wa CCM, lakini mbunge wa zamani wa Jimbo la Moshi Vijijini 2000-2005 NCCR-Mageuzi, anasema viongozi wa CHADEMA walishinikiza maandamano kwa sababu ya kifo cha hivi karibuni cha mwanachama wao, Ali Mohamed Kibao.

Kibao, mjumbe wa halmashauri kuu ya CHADEMA, alitekwa na kuuawa kisha mwili wake kupatikana Ununio nje kidogo ya Dar es Salaam. Alichukuliwa kwa nguvu kutoka kwenye basi na watu wenye silaha, waliosaidiwa na mwingine aliyejifanya abiria.

Mwili wake ulimwagiwa tindikali usoni kwa mujibu wa uchunguzi wa awali wa mwili wake.

"Maandamano ya amani ni haki kikatiba, lakini naamini hali ingekuwa tofauti kulingana na mazingira yaliyopo. Hivyo, polisi walikuwa na ulazima wa kuyazuia," anasema Ngawaiya.

Anafafanua kuwa, kwa matukio ya kutekwa au kuuawa kwa baadhi ya wanasiasa huku tuhuma zikielekezwa kwa polisi, kunaweza kuibua hasira na kusababisha watu kuumia na hata kushambuliwa.

"Kwa mfano, mtu anaweza kuua bila kukusudia, kwa kawaida polisi wanamweka ndani kwa ajili ya usalama wake, kwa sababu akiachwa mitaani, raia wanaweza kumuumiza," anasema.

Ngawaiya anasema, mazingira kama hayo ni sawa na tukio la maandamano ya CHADEMA yaliyopigwa marufuku, akisema iwapo wangeruhusiwa pengine wangeibua hasira kali kwa watu ambao huenda wameathiriwa kwa kupotea ndugu zao na kusababisha vurugu.

Kada huyo anasema, jambo la msingi ni kusubiri vyombo vya dola vimalize uchunguzi ili kuepusha mvutano usio wa lazima kati ya chama na taasisi hizo.

"Ni muhimu wanasiasa kuzingatia wakati sahihi wa kuandamana. Mbona wameandamana maeneo mbalimbali ya nchi huku wakilindwa na polisi, kwanini wanapozuiliwa wasiheshimu? Polisi hawawezi kuwazuia bila sababu. Wameona kuna viashiria hatarishi," anasema.

### NI HAKI LAKINI

Mchambuzi wa siasa Said Msonga, anasema pamoja na kwamba ni haki kikatiba kuandamana, pengine haukuwa wakati sahihi kwa chama hicho kuitisha maandamano.

Anasema, mvutano kati viongozi wa CHADEMA na polisi, ulitosha kwa chama hicho kutulia kwanza badala ya kulazimisha kuandamana wakati kukiwa na sintofahamu.

"Sijui maandamano yao yalilenga nini. Kama ni mauaji, serikali imeanza kuchukua hatua za uchunguzi, ingekuwa ni busara kusubiri kwanza," anasema Msonga.

Mchambuzi huyo anafafanua kuwa wana CHADEMA wangesubiri matokeo ya uchunguzi, na kuongeza kuwa wasiporidhika waitishe maandamano.

"Ingawa kuandamana ni haki ya kikatiba, sidhani kwamba ni sahihi kufanya hivyo, wakati uchunguzi ukiendelea, kwani ni sawa na kuzidisha mvutano usio wa lazima," anasema.

Msonga anasema, mivutano haileti muafaka, badala yake panapokuwapo sintofahamu, ni muhimu kukutana na kujadiliana ili kufikia mwafaka, kwa maslahi ya taifa.

"Maandamano yapo kikatiba, lakini yasilazimishwe pale linapojitokeza jambo ambalo halijawa sawa, badala yake limalizwe kwanza," anasisitiza.

### FALSAFA R4 KWANZA

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Bara, Magdalena Sakaya, anasema, falsafa ya R4 ya Rais Samia Suluhu Hassan ni vyema iheshimiwe.

INAENDELEA UK. 13

# Ziara ACT-Wazalendo mikoani inavyoibua madudu mapya



Kiongozi wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, akizungumza na wananchi katika moja ya mikutano ya hadhara. **PICHA: HALFAN CHUSI**

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kinaendelea na ziara katika maeneo mbalimbali, kikielezea kuibua mapya yanayofanywa na viongozi wasiowajibika na kutaka serikali iwachukulie hatua.

Wakuu wa chama hicho wamejigawa kikanda kufikisha salamu zao kwenye mikoa mbalimbali, wakieleza kuwa agenda kuu ya ziara hiyo ni kusajili wanachama wapya na kusikiliza kero za Watanzania.

Akiwa mkoani Tanga, Kiongozi wa Chama, Dorothy Semu, baada ya kulalamikiwa na wananchi kuwa hawalipwi kwa wakati wanapouza mazao yao, anamtaka Waziri wa Kilimo Hussein Bashe na Taasisi ya Kuzuia Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula NFRA.

Anapendekeza uchunguzi ufanyike ili kuujua ukweli na sababu ya wakulima kucheleweshewa malipo yao.

Anasema hata katika zama za kukua kwa teknolojia duniani inashangaza kuona zinapita wiki kadhaa mkulima hajalipwa, wakati mawasiliano nyakati hizi ni mepesi na pia kutuma pesa kielektroniki inawezekana.

Anasema walitegemea NFRA, ingemsaidia mkulima apate mahali salama pa kuuza mahidi yake, bei ya kuvutia ili afaidike na kilimo lakini wamepokea taarifa nyingi za namna wakulima wanavyonyanyasika.

"Mbona serikali haisikilizi shida za wananchi, tumesikia bunge linapitisha bajeti badala ya kupunguza mzigo wa kodi kwa wananchi limeuongeza. Tulikuwa tunalipia kodi ya majengo Sh. 1,000 sasa hivi ni Sh. 2,000 hiki ni kielelezo tosha kwamba imeshindwa kumtoa Mtanzania kwenye wimbi la umaskini.

"Ukiangalia maeneo mengi ya vijijini mambo ni yaleyale hakuna umeme, maji, shule na vituo vya afya. Hapa Tanga wananchi wamejitolea kujenga zahanati lakini hata kuwawekea umeme imeshindikana.

> Hata fidia wanazolipa bado ni ndogo, kuna mama ameniambia nyumba yake imebomolewa analipwa milioni 14 na hawajaambiwa kiwanja atapata wapi.

Anasema Tanga inaongoza kwa kilimo cha mahindi akikumbushia kuwa mwaka 2019-2020 mkoa ulizalisha zaidi ya tani 429.

Dorothy anawaomba Watanga kujitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wagombea wa chama hicho akisisitiza kuwa watakuwa kipaumbele kuwawezesha kujenga uchumi imara na kuhakikisha kila Mtanzania anafanya kazi na kupata ujira stahiki.

Dorothy anaeleza pia kuwa ACT-Wazalendo mpaka sasa imesajili zaidi ya wanachama wapya 20 na kwamba kazi inaendelea.

Akiwa mkoani Mtwara Katibu Mkuu wa Chama, Ado Shaibu, kwenye mkutano wa hadhara anaahidi kuwatetea na kukataa uovu hadharani na kwamba yupo tayari kufa akitetea haki.

Anasema takwa lao katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani ni atakayeshinda atangazwe sio kiongozi mmoja kutoa kauli ya nani atangazwe.

Anasisitiza kuwa hilo haliwezekani na kwamba wanataka haki itendeke ili uamuzi wa wananchi uheshimiwe. Kwa nyakati tofauti serikali na CCM vimekuwa vikisisitiza uchaguzi wa mwaka huu na mwakani utakuwa wa uhuru na haki akisema wanataka kuona maelezo hayo yakitimia.

Shaibu anawataka wananchi wa kusini kuwa mstari wa mbele kuwafichua wanaowanyonya kwenye kuuza mazao kuanzia ufuta, korosho na mbaazi.

"Msiwe wanyonge tupeni ushirikiano wa watu wanaowanyonya na kuwadhulumu haki zenu nipo tayari kusaidia. Tuacheni woga tutawaweka hadharani na hatua zitachukuliwa, kusini imegeuzwa kama chapati sekta ya kilimo inachezewa sana" anasema Shaibu.

Anawaambia wananchi wanaojitokeza kumsikiliza kuwa endapo chama chake kitashinda kitaondoa kero kwa wakulima.

Akiwa viwanja vya Karume Dar es Salaam Makamu Mwenyekiti wa Chama Bara Isihaka Mchinjita, anaishari serikali inaposanifu na kujenga barabara ijenge pia sehemu za biashara za wamachinga, kumaliza migogoro baina yao.

Ushauri mwingine anaoutoa ni kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya machinga katikati ya jiji ili kupunguza mwingiliano wa kibiashara. Anasema lengo ni kumaliza hisia kuwa Kariakoo ni mahali pa mapambano kati ya wafanyabiashara na Maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Akizungumzia wanaoondolewa katika bonde la Mto Msimbazi kulalamikia kutolipwa fedha kulingana na thamani ya eneo aliitaka serikali kurejea upya kwa wakazi hao kutatua changamoto hiyo.

"Tunafahamu mradi wa Benki ya Dunia umetoa zaidi ya Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kubadilisha sura ya Bonde la Mto Msimbazi lakini bado watu wanalipwa fedha kidogo.

"Hata fidia wanazolipa bado ni ndogo, kuna mama ameniambia nyumba yake imebomolewa analipwa milioni 14 na hawajaambiwa kiwanja atapata wapi." Anasema.

"Milioni 14 ni fedha ndogo sana kwa kiwanja kilichoko katikati ya jiji wakati leo ukivuka hapo Kigamboni kabla ya Mji Mwema kiwanja ni zaidi ya milioni 30."

Anaitaka serikali kurejea upya kinachoendelea katika bonde hilo na kuwashauri wananchi waliokataa kulipwa waingizwe kama sehemu ya wanahisa ili waweze kunufaika na mradi utakaojengwa hapo.

### KUMALIZA MIGOGORO

Akiwa Mbarali mkoani Mbeya, kiongozi mstaafu wa chama hicho, Zitto Kabwe, anataja mbinu za kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea na kusisitiza kuwa angekuwa kiongozi wa serikali angeimaliza ndani ya dakika 10.

Ato anazitaja mbinu atakazotumia kuwa ni pamoja na kutoa bikoni zilizowekwa katika makazi ya wananchi kuonyesha wapo ndani ya eneo la hifadhi.

"Kinachoitwa mgogoro wa ardhi ulipo Mbarali ni kitu kidogo tu, ni kuzitoa bikoni kutoka kwenye makazi ya wananchi na mashamba na kuzirudisha kwenye mpaka wa Hifadhi za Taifa (TANAPA), njia ni ndogo," anasema Zitto.

Mbinu nyingine, anaitaka serikali iunde tume ya kijaji, kwa ajili ya kupitia mipaka yote iliyokaribu na hifadhi na kuchora upya ramani ya matumizi ya ardhi na kuwashirikisha wananchi.

Zitto anasimulia uzoefu wake katika migogoro ya Mbarali kwamba alipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma ambayo jukumu lake lilikuwa kuchunguza kuhusu ubinafsishaji wa mashamba, kazi yao ya kwanza ilianzia mashamba ya Mbarali Estate na Kapunga.

"Moja ya jambo ambalo kila wakati ninalieleza kwa wananchi ni namna CCM ilivyoendesha ubinafsishaji. Tulipokwenda katika Kijiji cha Kapunga kukutana na wananchi, walitueleza, kuwa mwaka 1984, serikali iliwaomba ardhi.

Iliomba ardhi kwa ajili ya mradi wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), wakaipatia hekta 3,000 kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji. Ilipofika 1999 serikali ikashindwa kuendesha mradi huo". Anasema.

Anasema ikaamua kuubinafsisha na kukatangaza tangazo la kubinafsishaji kwamba wanabinafsisha hekta 3,500 wakati walipewa 3,000 na kwamba 500 ndio zilikuwa sehemu ya kijiji cha Kapunga. Zitto anasema alikwenda bungeni akaiuliza serikali imeamua kuwauza wanakijiji na mashamba yao?

Anakumbusha kuwa wakati huo bunge lilikuwa moto likapokea ripoti akaeleza alichoona Kapunga, Spika Samwel Sitta (sasa marehemu) akaagiza, yafanyike marekebisho ya mkataba wa mauzo, wanakijiji warejeshewe ardhi zao na ndivyo ambavyo kamati iliwaokoa wananchi wa Kapunga.

DIRA 2050

# Ndivyo madini ya kipekee yalivyo na nafasi kuipeleka nchi mbali kiuchumi

**Na Gaudensia Mngumi**

KATIKA kazi ya kukusanya maoni na kuandaa dira jumuishi ya maendeleo ya taifa 2050, moja ya maeneo ya msingi yanayotajwa ni kufikia mafanikio ya kuzalisha bidhaa muhimu duniani zenye lebo 'Made in Tanzania'.

Ni kazi ya dira ijayo kufanikisha kupata 'uzawa' au 'indigenizing' bidhaa za madini yanayochimbwa Tanzania kuchakatwa na kuyaongezea thamani ili taifa liendelee kupita rasilimali hiyo muhimu, inayopatikana kwa wingi nchini.

Ni kwa sababu eneo mojawapo linaloiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia ni utajiri wa madini yenye umuhimu wa kipekee kiuchumi yanayotengeneza viambato vya vifaa na bidhaa za kielektroniki, anasema Kamishna wa Madini mstaafu Dk. Peter Kafumu, Bidhaa hizo ni pamoja na simu, kompyuta, televisheni, ndege, roketi, magari, betrii za magari na vifaa vya kuzalisha umeme mbadala.

Anazungumzia madini hayo na jinsi dira ya maendeleo 2050 ilivyo na jukumu la kuyasimamia ili yanufaishe taifa, wakati huu yanapohitajika zaidi duniani kote.

Akizungumza na Nipashe anaeleza haya:

**SWALI: Ni nini maana ya madini yenye umuhimu wa kipekee?**

**JIBU:** Kitaalamu yanaitwa 'critical minerals', haya ni madini ambayo kiuchumi, kiviwanda na kiteknolojia yanahitajika zaidi.

Ni muhimu madini haya yakawekwa kwenye dira ya taifa 2050 ili taifa lifanye juhudi zote kuyachakata na kuyaongezea thamani hapa Tanzania, na ikiwezekana isitokee yakauzwa ghafi.

**SWALI: Kitu gani kifanyike kufikia azma hiyo?**

**JIBU:** Mosi tuandae wataalamu wa kuyafuatilia, kuyatafiti na kuyachimba.

Vyuo vya ufundi kama vya ufundi vya VETA, taasisi za teknolojia kama DIT, vikuu vya umma na vya binafsi viandae wataalamu na mafundi wa kusimamia kuchimba viwanda ili kuyaongezea thamani na kutengeneza vifaa mbalimbali.



Mtaalamu wa jiolojia na Kamishna wa Madini mstaafu, Dk. Peter Kafumu. **MPIGAPICHA WETU**

"Ni muhimu kila kitu kifanyike Tanzania kwa njia hiyo taifa liajiri vijana zaidi kuondoa ukosefu wa kazi. Lakini pia likusanye mapato zaidi na kuwekeza kwenye maendeleo.

Jingine ni kuvutia wawekezaji waanzishe viwanda, wafanye biashara na kuuza bidhaa za madini hayo popote zinapohitajika."

Tuzingatie kuwa na mazingira ya kuvutia uwekezaji kwa kutazama kwanza sheria zetu zivutie vitega uchumi vya Direct Foreign Investment (DFI).

Maeneo yenye migodi yaepushwe na migogoro. Yawekewe huduma muhimu kama ulinzi na usalama, maji, umeme, miundombinu, barabara, reli, madaraja na maghala.

Kingine pia kodi ziwe na mazingira viwe rafiki kuhamasisha mgeni kuchukua fedha zake na kutamani kuwekeza Tanzania na si kwingine.

**SWALI: Madini hayo ni yapi?**

**JIBU:** Baadhi ya madini hayo ni 'graphite ambayo ni muhimu kwenye kutengeneza betrii za magari yanayotumia umeme katika jitihada za kuachana na nishati chafu hasa mafuta.

Kadhalika graphite ni muhimu kwenye vinu vya kuchakata nyuklia. Yanahitajika kwenye kuzalisha vifaa vya kielektroniki kama simu janja, kompyuta zote, televisheni, ndege, vifaa vingi vya mawasiliano kama GPS na radar.

Pamoja na kazi hiyo yanatumiwa kuondoa joto ndani ya vifaa vya kielektroniki mfano simu, kompyuta na TV na kuyafanya kuwa na umhimu wa kipekee kwenye dunia ya kidijitali.

**SWALI: Yanapatikana wapi?**

**JIBU:** Yapo Morogoro -Mahenge, Lindi wilaya za Ruangwa na Mtwara kuna machimbo Masasi na Tanga pia kuna migodi.

Madini mengine ni shaba inayotumika kutengeneza nyaya za umeme ni muhimu kusafirisha umeme kwenye vifaa vyovyote. Inahitajika kwenye magari, meli, jenereta, nyaya za umeme majumbani kwa ujumlakwenye umeme shaba ni lazima.

**SWALI: Machimbo yako wapi?**

**JIBU:** Yanapatikana Kahama na iko kwenye makinikia ambayo kampuni ya Barick Gold inachimba. Mkoani Dodoma wilayani Mpwapwa na Mpanda mkoani Katavi.

Madini mengine yenye umuhimu wa kipekee leo ni 'nikeli' hii inachimbwa Kabanga mkoani Kagera.

Inatumiwa kutengeneza betrii za kuzalisha umeme kwenye magari ya umeme na vyombo vingine vya usafiri na kwenye vifaa karibu vyote vya kielektroniki.

Pamoja na Kabanga inapatikana Dutwa mkoani Simiyu, Nditi na Nachingwea mkoa wa Lindi ambako kuna hifadhi kubwa zaidi.

**SWALI: Kuna mkusanyiko wa madini yanayoitwa REE, tufafanulie ni yapi na wapi yanapopatikana.**

**JIBU:** REE ni kifupisho cha Rare Earth Elements -REE ni mkusanyiko wa madini ambayo ni muhimu yanayohitajika kwenye uzalishaji wa bidhaa za kiteknolojia.

Mfano kuna 'titanium, iridium ambayo hutumiwa kutengeneza vitu vya kielektroniki na vingine muhimu kama dira.

Kwa mfano iridium ni jamii ya chuma kisichoshika kutu wala kuchubuka kikikutana na hewa au unyevu ni madini ambayo yanapotumiwa kuunda vifaa havibabuki wala kuchubuka kwa kutu.

Aidha, tunapozungumzia 'titanium', ni muhimu kwanza ni madini ambayo ni mepesi yanatumika kwenye ndege, teknolojia za anga za juu na hata makombora yanayosafiri kwa kasi kwa sababu ya wepesi na uwezo wake wa kustahili joto au ubaridi mkali bila kuathirika.

Kadhalika madini mengine ndani ya REE yanatumiwa kutengeneza vifaa vinavyofua umeme kwenye paneli za nishati jua.

Ndani ya paneli kuna sumaku ndogo ndogo zinawekwa ili kunasa jua kuzalisha umeme. Ziko ndani ya mapanga au paneli hizo mahususi kunasa mawimbi ya jua na kufanikisha kutengeneza umeme jua.

Wakati wa kutengeneza vifaa vya kuzalisha nishati mbadala REE zina umuhimu mkubwa achilia mbali kuwa viambato vya vifaa vya kielektroniki kwenye viwanda vikubwa duniani.

**SWALI: Madini hayo yanapatikana wapi.**

**JIBU**: Taarifa zinaonyesha kuwa yapo kwa wingi nchini mfano kuna mgodi wa Ngwala mkoani Songwe.

Ndiyo maana tunashauri juhudi zote zifanyike kuhakikisha bidhaa zake na mnyororo mzima wa thamani unafanyika hapa Tanzania.

**SWALI: Unadhani kuna haja ya kuanza kuyachimba sasa au kusubiri mpaka taifa lijipange na kuwa na uwezo?**

**JIBU:** Kuna haja ya kuyachimba na kuuza lakini sambamba na uuzaji juhudi za kuanzisha viwanda vya kuyachakata na kuyaongezea thamani kiwe kipaumbele. Tuzifanye kwa bidii zaidi na dira iainishe na kufanikisha hilo.

## Kutoka Jicho la wachambuzi; CHADEMA na polisi kutunishiana misuli

**INATOKA UK. 11**

"Imenisikitisha kuona jinsi polisi walivyotumia nguvu kubwa kumdhibiti Mbowe wakiwa na bunduki kwa mtu asiye na hata kijiko mkononi bila kujali kwamba ni kiongozi mkubwa ana heshima yake," anasema.

Anasema, viongozi wa serikali wamsaidie Rais Samia kutimiza R4 kwa ustawi wa taifa, kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni nchi ya wote wakiwamo wanasiasa, wasio wanasiasa, wenye dini na wasioamini.

"Hakuna anayependa vurugu, kwa kuwa miezi ya hivi karibuni polisi walilinda maandamano ya CHADEMA, waendelee kufanya hivyo, badala ya kutumia nguvu kubwa kudhalilisha upinzani," anasema.

Mwanasiasa huyo anasema si sahihi polisi kutumia nguvu kubwa kwa jambo la kawaida na kufafanua kuwa wangemwita Mbowe kistaarabu ili kumtunzia heshima badala ya kumzingira wakiwa na bunduki.

"Inashangaza kuona Mtanzania ambaye hana silaha kuzingirwa kama mhalifu. Hebu tuheshimu falsafa ya Rais, iwe dira ya kuturudisha kwenye mstari," anasema Magdalena.

## JUKWAA LA VIONGOZI

# Mgogoro Israel Vs Hamas kuelekea kumaliza mwaka

• Wapalestina zaidi 40,000 wafa, wengi ni wanawake na watoto





Rais wa Iran, Ebrahim Raisi (kulia) na Kiongozi Mkuu wa Hamas, Ismail Haniyeh ni miongoni mwa viongozi wakuu wa Mashariki ya Kati waliouawa na Israel mwaka huu kwenye mgogoro wa Palestina na Hamas. **PICHA: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

NI takribani siku 353 tangu mgogoro kati ya Israel na kundi la Hamas la Palestina uanze Oktoba mwaka jana, ambao umekuwa ni vita visivyoisha.

Zipo athari za kiuchumi za moja kwa moja, achilia mbali za kijamii, mfano elimu, afya na mazingira vimeathiriwa na mgogoro huo ambao ulianza baada ya shambulio dhidi ya Isarel, likifanywa na Hamas Oktoba 7, mwaka jana.

Septemba 20, mwaka huu, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa(UN) linakutana kwa dharura mjini New York kufuatia mashambulizi ya Israel dhidi ya mji mkuu wa Lebanon wa Beirut na kusini mwa nchi hiyo.

Jeshi la Israel, limeshambulia Hamsas, baada ya Waisrael 1,200 kuuawa, huku 251 wakitekwa kwa mujibu wa BBC, inayoongeza kuwa takribani miili 10,000 imesalia kwenye vifusi vya majengo yalivyoshambuliwa kwa mabomu na makombora.

Mtoto Ali Ashraf Ata Gheith (15), anaiambia BBC kwamba ametumia takribani miezi miwili kufukua vifusi, kuangalia iwapo wanafamilia yake atawaona baada ya nyumba yao kusambaratishwa kwa bomu.

Wazazi, kaka na dada zake wawili wameuawa katika tukio hilo. Ali anasema bomu lilipopigwa alikuwamo ndani nyumba na kufukiwa na kifusi kwa zaidi ya saa saba kabla ya kuokolewa.

Anasema wakati anajitahidi kutoka katika kifusi hicho, mara kadhaa amejaribu kuchukua miili ya nduguze lakini ikashindikana.

> “Mwaka 2006, Hamas ilichukua utawala baada ya kupata ushindi katika uchaguzi wa bunge la Palestina, ingawa ushindi wake haukudumu kwa muda mrefu.



Rais wa sasa wa Iran, Masoud Pezeshkian.

“Nilimuona baba yangu chini ya kifusi sikuweza kufanya chochote, kwanza kwa sababu alikuwa chini ya nguzo mbili na paa lingeporomoka iwapo ningefanya chochote. Mwili wake ulioza mbele ya macho yangu,” anasema kwa huzuni Ali.

Wizara ya Afya, inayosimamiwa na Hamas, inasema miongoni mwa waliopoteza maisha tangu kuanza kwa vita hiyo inayowaita waathiriwa wakuu kuwa ni wanawake na watoto.

Inakadiriwa takribani Wapalestina 40,000 wameuawa tangu Oktoba 7, 2023 baada ya Hamas kuanza mashambulizi dhidi ya Israel, wizara hiyo inasema.

Idadi hiyo inatajwa kuwa ni asilimia 1.7 ya wakazi milioni 2.3 huku picha za satelaiti zinafanya uchambuzi zinabainisha kwamba karibu asilimia 60 ya majengo kwenye Ukanda wa Gaza yameharibiwa.

Hamas ni mojawapo ya makundi kadhaa ya wapiganaji wa Kipalestina ambayo yanadhibiti ukanda wa Gaza, inasema eneo hilo mara kwa mara hutumika kukabiliana na Israel. Itakumbukwa kuwa kundi hilo ndilo kubwa la Kiislamu miongoni mwa raia wa Palestina.

Shughuli zake za kisiasa tangu lilipoanzishwa limewekeza katika matawi mawili yenye malengo yasiyofanana; Kundi la wapiganaji wa Qassam, linalosimamia mapambano ya kivita dhidi ya Israel ambao uwepo wake haujatumbuliwa na Hamas na upande mwingine kuna kundi la kisiasa.

Mwaka 2006, Hamas ilichukua utawala baada ya kupata ushindi katika uchaguzi wa bunge la Palestina, ingawa ushindi wake haukudumu kwa muda mrefu.

Israel mara tatu imetekeleza mashambulizi dhidi ya wapiganaji wa Hamas, mfano ni mapigano ya Desemba 2008 yakifutiwa na ya Novemba 2012 na mengi yalikuwa Julai 2014.

Kampeni mbili za kwanza za Israel ziliathiri uwezo wa jeshi la Hamas, lakini kundi hilo, lilipata uungwaji mkono katika ukanda wa Gaza na eneo la West Bank kwa kusimama kidete dhidi ya Israel na kuendelea kustawi.

Vyanzo vya Palestina vinasema kwamba, kundi hilo la Kiislamu, lilijaribu kunyamaza baada ya operesheni ya pili ambayo ilisababisha vifo vya Wapalestina 170 wengi wao wakiwa raia pamoja na sita kati yao ni Waisrael katika siku nane.

Wapiganaji wa Qassam waliacha kurusha makombora ya roketi dhidi ya Israel, lakini kundi hilo, halikufanya chochote kuzuia makundi mengine ya Gaza kutekeleza mashambulizi yao, kwa kuwa halikutaka kuonekana kwamba halikupendelea vita dhidi ya Israel badala ya wapiganaji wengine hususan kutoka Islamic Jihad.

**BARAZA KUU UN**

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, limekutana wiki iliyopita katika kikao maalum cha dharura kuhusu Israel kuikalia kwa mabavu Gaza na Ukingo wa Magharibi ili kuzingatia rasimu ya azimio lililowasilishwa na Palestina ambalo pamoja na mambo mengine lingetaka kusitishwa kwa uvamizi huo ndani ya mwaka mmoja.

Zaidi ya wazungumzaji 90 wanasikilizwa wakati wa kikao hicho, na awali akifungua kikao hicho, Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Philemon Yang, anasema ni jukumu la Baraza Kuu na Baraza la Usalama kukomesha uwepo haramu wa Israel katika ardhi ya Palestina inayokaliwa kwa mabavu.

Utawala wa sheria na haki lazima uheshimiwe, anasema, kabla ya kumkabidhi Mwakilishi wa Kudumu wa Palestina katika Umoja wa Mataifa, Riyad Mansour, kuwasilisha rasimu yake ya azimio.

Nchi wanachama wamepanga kupigia kura rasmu hiyo Jumatano asubuhi New York, Marekani wakati kikao kitakapoendelea.

**VIKAO MAALUM**

Kwa mujibu wa azimio la Baraza Kuu namba 377A (V), “Kungana kwa ajili ya amani”, lililopitishwa mwaka 1950, wakati Baraza la Usalama, kutokana na kutoelewana kati ya wanachama wa kudumu, haliwezi kudumisha amani, kikao maalum cha dharura kinaweza kuitishwa “ndani ya saa 24 za wakati wa ombi la mkutano kama huo.”

Kikao maalum cha dharura kitaitishwa kwa ombi la Baraza la Usalama likiungwa mkono na kura za wajumbe wote saba wa baraza hilo, au kwa ombi la wanachama wengi wa Umoja wa Mataifa.



HABARI DODOMA

## RC ahimiza wananchi kujitokeza uboreshaji daftari

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wananchi kujitokeza kwenye uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura utakaoanza leo hadi Oktoba Mosi mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Senyamule alisema wanaohusika katika uboreshaji huo ni wananchi waliotimiza miaka 18 na watakaotimiza umri wa miaka 18 kabla ya siku ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

"Wengine ni wale walioijiandikisha awali na wamehama kata au jimbo moja kwenda lingine, wenye taarifa zilizokosewa wakati wa uandikishaji uliopita na waliopoteza kadi au kuharibika," alisema.

Alibainisha kuwa uboreshaji huo ni sehemu muhimu ya mchakato wa uchaguzi mkuu ujao na utahusisha kurekebisha taarifa, kuandikisha wapiga kura wapya na kuwaondoa kwenye daftari hilo waliokosa sifa.

"Wanaondolewa kwenye daftari hilo ni wale waliofariki, waliofungwa kifungo cha zaidi ya miezi sita na waliopata matatizo ya afya ya akili," alisema.

Kadhalika alisema uboreshaji huo pia utatoa fursa za wananchi kuhakiki taarifa zao kwenye daftari hilo ili kutimiza haki yao ya kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Alisema vituo vitakavyotumika katika uboreshaji wa vituo hivyo ni majengo ya umma kama vile ofisi za watendaji wa kata, mitaa, wenyeviti wa vijiji, vitongoji, shule na maeneo ambayo hakuna majengo ya umma.

Alisema Wilaya ya Dodoma kuna vituo 429, Bahi (191), Kongwa (229) na Chamwino (805) ambavyo vitakuwa vinafunguliwa kuanzia saa mbili asubuhi na kufungwa saa 12 ya jioni.

Alisema kwa wale watakaokuwa ndani ya kituo wataendelea kuandikishwa hadi waishe ndipo kituo kitafungwa.

Alisema Mkoa wa Dodoma unakadiriwa kuwa na wapigakura 1,777,834 kati ya hao wapo ambao hawajawahi kujiandikisha ambao ni 845,976.

# Daktari aeleza mbinu za kuepuka shinikizo la damu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAKAZI wa Dodoma na mikoa yenye maji ya chumvi wameshauriwa kutoweka chumvi nyingi kwenye chakula ili kuepuka kupata ugonjwa wa shinikizo la damu.

Aidha, Watanzania wameshauriwa kila wanaposherehekea siku zao za kuzaliwa wajenge utaratibu wa kupima ugonjwa huo.

Ushauri huo umetolewa na Daktari Bingwa wa Upasuaji, Dk. Mugisha Nkoronko wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Dk. Mugisha ambaye ni Makamu wa Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) alisema tatizo la shinikizo la damu ni kubwa, hivyo wameamua kutoa huduma ya bure kwa siku mbili jijini Dodoma ili wananchi wapate ushauri pamoja na matibabu ya magonjwa hayo.

"Kuweni makini kwenye maandalizi ya chakula, hususani kuweka chumvi nyingi kwenye vyakula hasa katika mikoa yenye maji ya chumvi maana chumvi ni chanzo kimoja wapo cha shinikizo la damu, hivyo tunapaswa kuwa makini katika uandaaji wa vyakula vyetu vya kila siku," alisema.

Alisema bado kuna watu wanachelewa kuanza matibabu wakidhani ugonjwa huo unatokana na imani za kishirikina jambo ambalo siyo kweli.

Alisema ugonjwa wa shinikizo la damu unatibika endapo watu watafuata masharti yanayotolewa lakini pia kuangalia namna ya ulaji wa vyakula mbalimbali.

Pamoja na hayo alihimiza wananchi kujenga tabia ya kupima maradhi ya moyo ili kujua hali zao mapema na kuanza matibabu.

Alisema: "Kuna kila sababu ya watu kuwa makini kwenye suala la ulaji wa vyakula, lakini pia watu wajitahidi kufanya mazoezi ili kuweka afya zao vizuri kulingana na ratiba za vyakula wanavyokula".



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa mkoa huo, unaotarajiwa kuanza leo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mradi kuzuia vitendo vya ukatili waanza

**Na Paul Mabeja,**
CHAMWINO

KUTOKANA na kukithiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia nchini, Taasisi ya Foundation For Disabilities Hope (FDH) imeanza kutekeleza mradi wa kuzuia vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto wenye ulemavu.

Akizungumza jana wilayani hapa, wakati wa mafunzo ya namna ya kukabiliana na vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto wenye ulemavu, Mratibu wa mradi wa chukua hatua sasa zuia ukatili, Glory Mbowe alisema lengo ni kuzuia vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto wenye ulemavu.

"Lakini pia malengo mahususi ni kutoa elimu juu ya masuala ya ukatili na haki za binadamu ili wanawake na watoto wenye ulemavu waweze kutambua haki zao za msingi lakini pia kuwajengea uwezo wanawake na watoto wenye ulemavu kuripoti vitendo vya ukatilii kwenye vyombo husika," alisisitiza Glory.

Aidha, alisema mradi huo ambao unatekelezwa katika Wilaya ya Chamwino katika Kata ya Buigiri utatumika pia kutoa mafunzo ya namna gani watu wenye ulemavu wanaweza kukabiliana na vitendo vya ukatili.

"Mafunzo haya yatasaidia kuongeza uelewa kwa wanawake na watoto wenye ulemavu kuwa na uwezo wa kutambua haki zao za msingi na pale wanapofanyiwa ukatili ni hatua gani wachukue ili kuondokana na kadhia hiyo," alisema Glory.

Mwezeshaji katika mafunzo hayo kutoka Dawati la Jinsia Kituo cha Polisi Wilaya ya Chamwino, Malale Michael, alisema moja kati ya vitu ambavyo wanawafundisha wanawake na watoto wenye ulemavu ni kujua maana ya ukatili.

"Tunawafundisha kwanza kujua ukatili ni nini, lakini pia upo wa aina gani lakini wakishajua wanawezaje kutoa taarifa za matukio ya ukatili ili vyombo husika viweze kuchukua hatua na kukomesha vitendo hivyo," alisema Malale.

Aidha, alisema Wilaya ya Chamwino bado inakabiliwa na matukio ya ukatili ikiwamo ndoa za utotoni pamoja na ulawiti na ubakaji.

"Hali ya vitendo vya ukatili katika wilaya hii siyo mbaya sana wala siyo nzuri sana lakini matukio haya bado yapo na sisi kama Jeshi la Polisi tumeanzisha kampeni ya kuzuia hali hiyo inayosema tuchukue hatua mapema," alisema.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kutumia nyumba za ibada ili kuwapa uelewa wananchi kuhusu vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto wenye ulemavu.

Mwanasheria wa FDH, Joyce Mhana alisema kwa mujibu wa Katiba kila binadamu ni sawa, hivyo hakuna sababu ya mtu kumfanyia ukatili wa aina yoyote.

Alisema: "Lakini pia ipo Sheria Namba 9 ya Mwaka 2010 ambayo inasema kuwa watu wenye ulemavu wanapaswa kulindwa na inatoa wajibu kwa watu wengine kumlinda na kwa yule ambaye ataoneka kushindwa kutimiza na yeye atachukuliwa hatua kama ni sehemu ya wanaofanya ukatili huo".





# Mbolea ya ruzuku tani 60,000 kutoka Zambia yawasili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeanza maandalizi ya msimu mpya wa kilimo cha tumbaku kwa kuingiza tani 60,000 za mbolea ya ruzuku kutoka Zambia, kwa ajili ya kuwarahisishia wakulima upatikanaji wa bidhaa hiyo.

Uagizaji wa mbolea hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwa Wizara ya Kilimo alilolitoa hivi karibuni la kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati ili waendane na msimu wa kilimo.

Akipokea shehena hiyo, Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema magari zaidi ya 170 yaliyobeba bidhaa hiyo yameshawasili nchini na kwamba hiyo ni awamu ya kwanza kulingana na makubaliano waliyoingia ya uagizaji.

Alisema awamu hiyo ni kwa ajili ya mbolea ya tumbaku na baada ya hapo wataanza kuingiza mbolea zingine kwa ajili ya kilimo cha mazao mengine yakiwamo ya chakula.

Alisema wizara hiyo itaendelea kutekeleza maagizo ya Rais Samia ya kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo za kilimo kwa wakati na hivyo akawahakikishia wakulima wote watapata mbolea ya ruzuku kabla ya mvua kuanza.

"Leo tuko hapa Mbeya kupokea mbolea ya ruzuku, haya ni maelekezo ya Rais Samia na sisi tumeshatimiza maelekezo yake tunamkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ili ahakikishe usalama wa mbolea hizi na ziwafikie wakulima wote," alisema Silinde.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Samuel Mshote, alisema mbolea iliyowasili nchini inatosha mahitaji ya wakulima tumbaku, hivyo wanapaswa kuitumia fursa hiyo kuhakikisha wanaongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo nchini.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 serikali imeelekeza TFC kuagiza mbolea tani 130,000 kutoka Zambia, hivyo kuwasili kwa tani hizo kwa ajili ya wakulima wa tumbaku ni sehemu ya tani hizo.

"Kwa sasa tuwaombe wakulima kuchangamkia mbolea hii haraka, wainunue mapema ili kujiandaa na msimu mpya wa kilimo ambao utaanza muda siyo mrefu," alisema Mshote.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema kwa muda mrefu wakulima wa tumbaku wamekuwa wakilalamikia kutoguswa na mpango wa mbolea ya ruzuku, hivyo kuletwa kwa mbolea hiyo kumejibu malalamiko ya wakulima hao.

Alisema kwa msimu ujao Mkoa wa Mbeya unatarajia kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka tani 24,000 za msimu uliopita hadi tani 30,000.

Hata hivyo alisema tayari wameandaa utaratibu mzuri wa kusambaza mbolea hiyo kwenye vyama vya msingi na kuhakikisha inawafikia wakulima wa vijiji vyote na kuwataka wakulima wa tumbaku kuondoa hofu kwani kila mmoja atafikiwa kulingana na utaratibu uliopangwa.

## Viongozi CCM Wanging'ombe wakumbushwa wajibu wao

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe wametakiwa kutokaa kimya bali wawaeleze wananchi mafanikio yaliyofanywa na serikali, husani kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, wakati wa mkutano wa kuwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi Julai 2024.

Alisema katika kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wanachama wanapaswa kufanya tafakuri sahihi kuhusu chaguo la viongozi wanaowatarajia.

"Tukumbuke sisi tunauza maendeleo na tuwaambie wananchi maendeleo yaliyofika tusiwe wepesi wa kusahau bali tukumbushe kwa sababu ndiyo tunaopiga nao kampeni," alisema Prof. Mkenda.

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji, Mbunge wa Wanging'ombe, Dk. Festo Dugange, alisema ilani ya uchaguzi imetekelezwa vyema kutokana na serikali kuwa sikivu katika kutatua kero mbalimbali kwa wananchi.

"Nasimama mbele yenu viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi, kumshukuru sana Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha, katika kipindi cha mwaka 2021 tukajenga Shule ya Sekondari Kidugala ambayo imekamilika na inatoa huduma," alisema Dk. Dugange.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Wang ing'ombe, Frank Chaula, alisema wamefanya ziara kwenye matawi na kuona miradi mingi inaendelea kufanyika pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zacharia Mwansasu, aliwataka viongozi wa chama, wananchi pamoja na watumishi kutunza miradi hiyo kwa sababu serikali imetoa fedha kwa ajili ya kuitekeleza.

Mmoja wa wajumbe walioshiriki mkutano huo, akiwamo Eliza Mdapo alisema katika maeneo ya vijijini tayari umeme umefika na hivyo kuwarahisishia katika shughuli zao za kiuchumi ikiwamo kuchomelea vyuma.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Kailima Ramadhani, akizungumza na washiriki wa mafunzo ya waandishi wasaidizi na waendesha vifaa vya Bayometriki (BVR), watakaohusika na zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, jijini Dodoma juzi. Mzunguko wa tano wa uboreshaji wa daftari hilo, utajumuisha Halmashauri ya Jiji hilo, Wilaya ya Bahi, Chamwino na Kongwa na kwa mkoa wa Manyara ni Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Kiteto na Simanjiro. **PICHA: INEC**

# Wafugaji wavamia eneo la mradi wa soya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

BAADHI ya wafugaji wanadaiwa kuvamia eneo la mradi wa kilimo cha soya katika Kijiji cha Mapogoro wilayani Chunya mkoani Mbeya, hali ambayo inaweza kukwamisha utekelezaji wa mradi huo.

Wafugaji hao wanadaiwa kuhamia katika eneo hilo kinyemela wakitokea katika kitongoji cha wafugaji kilichoko jirani na eneo hilo ambacho kina maeneo mawili ya makazi ya wafugaji ambayo ni Masiano na Mbanga.

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarak Batenga, aliwataka wafugaji hao kuondoka katika eneo hilo na kurejea kwenye maeneo yao kabla serikali haijaanza kuwachukulia hatua.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wakazi wa kijiji hicho, Batenga alisema serikali imetoa ekari 50 kwa kila kaya na kutoa hati miliki katika eneo lililoko msitu wa kijiji ili kupisha utekelezaji wa mradi huo, hivyo akawataka waliovamia eneo la mradi kuondoka mara moja.

Alisema wananchi wa Kijiji cha Mapogolo ndiyo wanufaika wa kwanza wa mradi huo utakapoanza utekelezaji mpaka ukamilika, hivyo wanapaswa kulinda usiendelee kuvamiwa na watu wenye nia ovu.

"Niwasihi wakazi wa vijiji hivi ambavyo mradi upo hasa vijana kujipanga vyema kushiriki kwenye mradi huu ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi," alisema Batenga.

Katika hatua nyingine, aliwataka wananchi hao kuheshimu mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao wameupitisha kwenye mikutano yao ya kijiji ili kuondokana na migogoro ya ardhi na kuipa nafasi serikali kuwaletea maendeleo.

Wakizungumza kwenye mkutano huo wananchi hao walioomba serikali kutatua matatizo yaliyoko kijijini hapo ikiwamo ubovu wa barabara, upungufu wa madawati, ukosefu wa umeme, majisafi na salama pamoja kukosekana kwa zahanati ya kijiji hali inayowalazimu kufuata huduma vijiji vingine.

Hata hivyo Mkuu huyo wa Wilaya aliwahakikishia wananchi hao kupitia ujio wa mradi huo wa kilimo cha soya serikali itapeleka huduma zote muhimu za kijamii ikiwemo kujenga barabara, umeme na maji, kujenga zahanati, shule pamoja na huduma nyingine zote za kijamii.

Wilaya ya Chunya imetenga mashamba ya ekari 52,000 kwa ajili ya kilimo, kwamba ekari 27,000 zipo eneo la Mapogoro, ekari 11,000 zipo katika Kata ya Nkung'ungu na ekari 13,000 eneo la Lualaje.





## Ujenzi majengo ya mahakama wafikia 45%

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya Zanzibar imesema kasi ya ujenzi wa majengo ya mahakama za mkoa na wilaya kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) umefikia asilimia 45.

Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ufanisi wa usikilizaji wa mashauri yanayowakabili wananchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa maagizo yaliyotakiwa kufanywa na Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023-2024 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu miongoni mwa vipaumbele vya serikali ni kuona mfumo wa usikilizaji wa kesi unapatiwa ufumbuzi ikiwamo kuajiri mahakimu na majaji wa kutosha.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu zaidi ya majaji 10 wameteuliwa kushika wadhifa huo, hatua ambayo imesaidia kuwepo kwa usikilizaji wa mashauri yanayowakabili wananchi kwa kasi kubwa.

Aidha, alisema mahakama maalumu ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto imeanzishwa ambayo imesaidia kuwepo kwa kasi ya usikilizaji wa kesi zinazohusu kundi hilo.

Alisema kwa mara ya kwanza katika Kisiwa cha Pemba yupo Jaji wa Mahakama Kuu anayesiliza kesi zinazohusu matukio ya mauaji pamoja na rufaa zinazowahusu wananchi, hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuondosha malalamiko yaliyokuwepo awali.

Kadhalika, alisema Serikali ya Zanzibar imeanza uchunguzi wa miradi ya maendeleo 70 na kubaini kuwepo kwa kasoro za kiutendaji zinazohusu ubadhirifu wa mali ya umma.

Akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir aliyetaka kujua kazi za uchunguzi zinazofanywa na Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) katika miradi ya maendelezo zimefikia wapi.

Waziri Suleiman alisema serikali imejipanga kuhakikisha miradi yote ya ujenzi wa maendeleo inafanyiwa uchunguzi kuona fedha halisi na thamani yake inavyozingatia ubora wake.

Alisema miradi 72 ya maendeleo yenye thamani ya Sh.bilioni 784 imefanyiwa uchunguzi na kutolewa ushauri baada ya kuonekana kasoro mbali mbali za ujenzi wake.

Alisema miradi mitano imebainika kuwa na kasoro ambazo zimebainika kuwepo kwa maosa ya kijinai, kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika wake.

# Serikali yanunua 'drone' ukaguzi hifadhi za misitu

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

KATIKA kukabiliana na matukio ya uvamizi na uharibifu wa ukataji wa miti hasa katika maeneo ya hifadhi za misitu, Serikali ya Zanzibar imenunua ndege mbili zisizokuwa na rubani kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa maeneo hayo.

Ndege hizo zitafanya doria katika Msitu wa Hifadhi ya Taifa Jozani Unguja na Ngezi Pemba.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, wakati akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa wizara hiyo inayotokana na maagizo ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Biashara Utalii na Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema serikali imechukua uamuzi huo kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa misitu katika hifadhi hiyo, kwamba uchunguzi uliofanywa umebaini kuwapo kwa athari kubwa za uharibifu wa kimazingira.

Alisema watu wasiofahamika kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiingia ndani ya hifadhi ya misitu hiyo na kukata miti kwa matumizi mbalimbali ikiwamo ya mkaa na kupasua mbao kinyume na sheria.

Alisema serikali imechukua juhudi kubwa za kuimarisha Hifadhi ya Misitu ya Jozani na Ngezi ambapo kwa nyakati tofauti wananchi wanaozungukwa na hifadhi hiyo wamekuwa wakipata mgawo wa fedha zinazotokana na mapato kutoka kwa watalii na wageni wanaotembelea hifadhi hizo.

Alisema katika Msitu wa Hifadhi ya Ngezi tayari wanavijiji sita wanaozungukwa na hifadhi hiyo kwa nyakati tofauti wamepata mgao wa Sh.milioni 30 zinazotokana na mapato ya watalii kutembelea maeneo hayo.

Alisema asilimia 30 ya mapato yanayotokana na Hifadhi ya Ngezi yanakwenda kwa jamii ambao ni wanavijiji wanaozungukwa na hifadhi hiyo, huku asilimia 50 inakwenda serikalini.

''Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba wizara imechukua juhudi za makusudi kupambana na uharibifu wa hifadhi za misitu ya taifa kwa kununua ndege mbili zisizokuwa na rubani ili kukabiliana na uhalibifu," alisema.

Aidha, Shamata aliwapongeza wananchi wa maeneo yanayozungukwa na Msitu wa Hifadhi ya Ngezi kwa kuanzisha jumuiya inayosimamia uhifadhi iitwayo NGERARECO ambayo imesaidia kupambana na uhalifu na kulinda hifadhi hiyo.

Hata hivyo alisema serikali inaendelea na juhudi zake za kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji shambani baada ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa miundombinu katika mabonde manne ya Unguja na Pemba.

Aliyataja mabonde ya mpunga yaliyokamilika kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mpunga wa umwagiliaji maji ikiwemo Cheju Wilaya ya Kati Unguja na Kibokwa.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Bajeti 'kusapoti' vyuo vikuu kufanya utafiti yaandaliwa

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman amesema atahakikisha kunatengwa bajeti maalum ya kuwezesha taasisi za elimu ya juu kwa ajili ya kufanya utafiti nchini.

Alisema hayo juzi wakati akifungua Kongamano la Miaka 60 ya Elimu Bila Malipo iliyofanyika katika Chuo cha Utalii kilichopo eneo la Maruhubi.

Alisema kufanya hivyo ni kuifanya nchi kuwa na utafiti nyingi ambazo zitaisaidia katika kupanga maendeleo.

Aidha, aliwataka walimu kuwa wazalendo, watiifu na usimamizi katika kazi zao za kila siku kwa kuhakikisha wanawasimamia vyema wanafunzi ili kuleta ufaulu mzuri.

Waziri huyo aliwataka vijana na wananchi kudumisha amani na utulivu kwa kusimamia vyema masuala ya elimu na kuepuka vishawishi ambavyo vitahatarisha uvunjifu wa amani.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha maendeleo ya elimu kwa kufanya mageuzi makubwa ambayo yataendana na mabadiliko yaliyopo ulimwenguni.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa, alisema serikali inachukua jitihada kubwa kuhakikisha inalipia gharama zote ili kila mwananchi apate elimu.

Alisema kwamba katika kipindi cha miaka 60 ya elimu bila malipo serikali imeimarisha usomaji kwa kuwajengea wanafunzi maktaba za kisasa ambazo zitakuwa na vifaa vya kutosha vya kujifunza.

Alisema kwa mwaka 2024 Zanzibar ina shule za serikali na binafsi 1, 138 zinazotoa elimu katika ngazi maandalizi zenye wanafunzi 103, 581.

"Takwimu zinaonesha kuwa shule 707 zinatoa elimu ya msingi ambapo ujumla ya wanafunzi 391, 338 wanapata elimu hiyo" alisema Lela.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Taifa (SUZA), Mohamed Makala Haji, alisema Zanzibar kwa miaka mingi kabla ya mapinduzi walikosa nafasi ya kupata elimu katika ngazi mbalimbali.

Alisema hivi sasa serikali imetilia mkazo suala la elimu bila malipo kwa kuhakikisha inaimarisha masuala ya elimu, uchumi na michezo.

Alisema SUZA imetanua wigo kwa kutoa taaluma ya utafiti lakini pia kutoa ushauri elekezi kwa maeneo mbalimbali ya utaalamu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SOPHIA MORIS COSTA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5482.0030** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MANUS DEI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **TAB/RB/6888/023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIA CHARLES NYANDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0264-0035** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BARBRO JOHANSSON GIRLS SCHOOL** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/197158/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOHN LYAHASI EMMANUEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3039/0185 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHAMALIWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 na cheti cha chuo cha **BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN PUBLIC SECTOR ACCOUNTING AND FINANCE** chenye usajili namba **DSM/BTCPSAF/18/54876** kilichotolewa na **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DOD/DOD/RB/344577/2021,DOD/DOD/RB/344590/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**REMIDIUS EDWINI NICKSON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3158/0089/2020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KANAZI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MWA/ILE/24186/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MASOUD JUMA NGALAGALE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1186/0610** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAKITA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/KIG/UVI/3023/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABDULKARIM AYOUB KAMTI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2549-0022** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALPHA HIGH SCHOOL** mwaka 2014 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0867- 0511** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **PANDAHILL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarif kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/205674**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ELIZABETH CHARLES JOSEPH** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki **MAKERA INVESTMENT COMPANY LTD** yenye usajili namba **MC 403 BUT.** Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/SHI/KAH/7743/2024**

## KUPOTEA HATI YA NYUMBA

Ndugu **ALLY HASSANI MWANGA** anatangaza kupotea kwa Hati yake ya Nyumba **Plot No. 7 block 101** barabara ya 15 Ngamiani.

Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.

Amefika Polisi na amepewa Loss Report.

Taarifa Polisi:

**PHQ/TAN/TAN/10185/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NYAMTONDO G KASORI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 456 BKC.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

POLISI TAARIFA:

**PHQ/MWA/NYA/20971/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 23593/2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE OBED MWAKASUGULE SALAKA**

**AND**

**In the matter of Application for letters of Administration by SADICK O. SALAKA.................................................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23rd of October 2024.

Dated at Kyela this 23rd day of September, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

KYELA.

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki na wakurugenzi wa kampuni ya **TANZANIA HOME $ OFFICE MAIDS SERVICES LIMITED** yenye namba za usajili **156737046,** wanapenda kuutangazia umma kua kutokana na kushindwa kujiendesha, wamiliki wameamua kuifunga [kwa mujibu wa sheria za BRELA. Hivyo tunaomba kama kuna mtu yoyote ana pingamizi, malalamiko au madai yoyote awasiliane kwa njia zifuatazo.

Email: **ernestrosemary145@gmail.com**

Rosemary Ernest Kasunzu
Mkurugenzi Mtendaji

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA NZEGA**

**MAOMBI MADOGO NA. 16 NA 17 YA MWAKA 2024**

1. **MASUNGA MOHAMED**
2. **MALOMO MOHAMED**
3. **AMOS MOHAMED**
4. **KALIWA MOHAMED ..............................WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **JUDITH HAULE (Mirathi ya Marehemu MOHAMED KALIWA MALOMO)**
2. **SHIMBA MOHAMED......................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi **SHIMBA MOHAMED** popote ulipo unafahamishwa kwamba **MASUNGA MOHAMED . NA WENZAKE** 3 wamefungua maombi Madogo Na. 16 & 17 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lililopo Nzega. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 25/09/2024 saa 2:30 asubuhi. Hivyo mnatakiwa kuleta utetezi wenu ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya kutolewa tangazo hili. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba (W) – Nzega. Ufahamu kwamba usipohudhuria maombi husika yatasikilizwa bila yaw ewe kuwepo /kutoa utetezi wako na kutolewa hukumu.

**IMETOLEWA** na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 23/09/2024.

V. A.LINGWENTU
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
NZEGA

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 23625 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LAMECK ISRAEL MKUVASA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AGATHA MICHAEL SEMPOMBE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admionistration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18th day of October 2024

Dated at Korogwe this 23rd of September 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 21483/2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ZAWADI KIBWEJA MTEMBEZI**

**AND**

**In the matter of Application for letters of Administration by RONIKA NTENGO IPAJA.........................................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 4th of October 2024.

Dated at Kyela this 23rd day of September, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

KYELA.

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0677 020701*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Israel yawafukuza raia kusini mwa Lebanon

**JERUSALEM,** Israel

JESHI la Israel limewataka wakazi wa kusini mwa Lebanon kuyahama makazi yao mara moja kutokana na kile ilichokisema yanatumiwa na kundi la Hezbollah kuhifadhi silaha na kwamba itafanya mashambulizi makali katika eneo hilo.

Ilielezwa kuwa tahadhari hiyo kutoka kwa Jeshi la Israel ni ya kwanza na ya aina yake katika kipindi cha takriban mwaka mmoja wa mzozo unaozidi kuongezeka katika eneo hilo la Mashariki ya Kati, ikielezwa kuwa imetolewa baada ya majibizano makali ya mashambulizi yaliyofanyika juzi.

Ilielezwa kuwa siku ya Jumapili Hezbollah ilirusha takriban makombora 150 pamoja na droni kuelekea kaskazini mwa Israel ikiwa ni mashambulizi ya kulipiza kisasi baada ya kuuliwa kwa kamanda wake pamoja na wapiganaji wengine.

Vyombo vya habari vya Lebanon vilisema kuwa wakazi katika eneo hilo wamepokea ujumbe wa maandishi wakihimizwa kuondoka katika majengo ambayo Hezbollah huyatumia katika kuhifadhi silaha.

Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari alisema kwa zaidi ya kipindi cha miaka 20 kundi hilo limekuwa likitumia makazi ya raia kuficha silaha zake na lengo la operesheni hiyo ni kuziteketeza silaha hizo.

"Hiki ni kijiji cha kusini mwa Lebanon, Hezbollah wanahifadhi makombora, roketi, silaha ya kufyatulia makombora ndani ya nyumba za raia," alisema Hagari.

Aliongeza kwamba katika operesheni ambayo wamepanga kuifanya italenga kuzisaka na kuziharibu silaha zote.

Aidha, haikuweza kubainika hasa ni watu wangapi ambao wameathirika na amri hiyo ya Israel, na kwamba idadi kubwa ya jamii zinazoishi maeneo ya mpakani zimehamishwa kutokana na kushuhudiwa kwa mashambulizi ya mara kwa mara.

Waziri wa Ulinzi wa Israel Yoav Gallant alisema wataendeleza na utekelezaji wa mashambulizi nchini Lebanon hadi pale watakapotimiza malengo yao na kuhimiza utulivu ndani ya Israel katika wakati huu.

Kuongezeka kwa majibizano ya mashambulizi kutoka kila upande kumeongeza hofu ya kutanuka kwa mzozo huo katika wakati huu ambako jeshi la Israel bado linapambana na kundi la Hamas huko Gaza, ikijaribu kuwarejesha mateka waliochukuliwa baada ya shambulio la Oktoba 7.

Hata hivyo, kundi la Hezbollah limeapa kuendeleza mashambulizi yake iliyoyataja ya kuonesha mshikamano kwa Wapalestina na Hamas.

Kikosi cha kulinda amani cha UNIFIL kusini mwa Lebanon kupitia kwa msemaji wake Andrea Tenenti, alisema kumekuwa na ongezeko la mashambulizi ya mabomu katika eneo lote la operesheni hasa katika sehemu za mpaka wa Israel na Lebanon.

Mashambulizi hayo yanafanyika huku kukiwa na mapigano makali zaidi kwa takriban mwaka mmoja wa mzozo unaoendelea kusambaa na vita kati ya Israel na Hamas huko Gaza.

Kando na Lebanon, mashambulizi makubwa ya vikosi vya Israel katika moja ya kambi ya wakimbizi yamesababisha vifo vya Wapalestina kumi wakiwamo watoto wanne katika eneo la Ukanda wa Gaza jana.

Mashambulizi hayo yanafanyika katika wakati ambapo hadhari ya kimataifa imeugeukia mzozo wa Lebanon kati ya Israel na kundi la Hezbollah. **DW**



Vikosi vya uokoaji vya Israel vikizima moto baada ya shambulio la Hezbollah kaskazini mwa nchi hiyo jana. **PICHA: MTANDAO**

## Misri yaipatia silaha Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

MAOFISA wa usalama katika mji mkuu wa Mogadishu wamesema meli ya Misri imewasilisha shehena kubwa ya vifaa vya kijeshi nchini Somalia, huku Waziri wa Ulinzi katika taifa hilo, Abdulkadir Mohamed, akiishukuru Misri kwa hatua hiyo.

Ilielezwa silaha hizo zilifikishwa Somalia jana, na kwamba hiyo ni mara ya pili kwa silaha kutolewa kwa namna hiyo kutoka Misri katika kipindi cha mwezi mmoja huku mahusiano yakizorota kati ya Somalia na Ethiopia.

Ilielezwa kuwa Misri ni mpinzani wa muda mrefu wa Ethiopia, na kwamba imechukua fursa hiyo kusogea karibu na Somalia, na kuzua wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa mvutano katika upande wa Afrika.

Shirika la habari la Reuters likinukuu maofisa wa usalama na bandari, walisema shehena hiyo ya kijeshi, iliyobebwa kwenye meli ya kivita iliyowasili Somalia, ilijumuisha bunduki za kupambana na ndege na mizinga.

Katika taarifa aliyoitoa kupitia mtandao wake wa X Waziri Mohamed alisema "Somalia imepita hatua ambako itaamrishwa na kusubiri ruhusa ya wengine juu ya nani itashirikiana naye. Tunajua maslahi yetu wenyewe, na tutachagua kati ya washirika wetu na adui zetu, asante Misri".

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Ethiopia kwa miaka mingi imekuwa muungaji mkono mkubwa wa serikali mjini Mogadishu katika mapambano yake dhidi ya kundi la wanamgambo wenye mafungamano na al-Qaeda na al-Shabab.

Lakini Somalia ina hasira kwamba Ethiopia isiyokuwa na bandari ilitia saini makubaliano ya awali mwanzoni mwa mwaka huu na jimbo la Somaliland lililojitangazia uhuru kukodisha sehemu ya ufuo wake. Huku Somalia ikiiona Somaliland kama sehemu ya ardhi yake.

Wakati huo huo, Ethiopia ilielezea wasiwasi wake kwamba shehena ya silaha na vikosi vya kigeni inaweza kuzidisha hali ya usalama katika nchi ya Somalia. **BBC**

# Mawakili wapinga usitishaji wa uchaguzi Sudan Kusini

**JUBA,** Sudan Kusini

KUNDI la mawakili wa Sudan Kusini wamewasilisha kesi katika mahakama kuu ya nchi hiyo kupinga kuahirishwa kwa uchaguzi wa rais na kuongeza muda wa serikali ya mpito kwa miaka miwili.

Siku chache zilizopita, ofisi ya Rais Salva Kiir ilitangaza kuongeza muda wa kipindi cha mpito kwa miaka miwili na kuahirisha uchaguzi kwa mara ya pili kufuatia kucheleweshwa kwa 2022.

Ilielezwa kuwa mwishoni mwa wiki jana, bunge liliidhinisha uamuzi huo bila mabadiliko baada ya baraza la mawaziri kuuidhinisha. Licha ya kwamba uchaguzi ulipaswa kufanywa Desemba mwaka huu.

Iliekezwa kuwa jana mawakili hao waliopinga hatua hiyo walienda kwa Mahakama ya Juu, wakiiomba itangaze kuwa tangazo hilo ni batili na liko kinyume na katiba.

Wakili Deng Deng, akizungumza kwa niaba ya wenzake, aliwaambia waandishi wa habari muda mfupi baada ya kufungua kesi hiyo kwamba "Kama mawakili, tunadhani kwamba muda huu wa kuongeza muda ni kinyume na katiba, ni kinyume cha sheria na tunaitaka serikali yetu kufanya uchaguzi ndani ya muda uliopangwa".

Michael Makuei, waziri wa habari na msemaji wa serikali, hakujibu mara moja ombi la maoni.

Kuahirishwa huko kuliwafanya wadhamini wa kimataifa wa mchakato wa amani wa Sudan Kusini kueleza kusikitishwa kwao, wakisema kulionyesha kushindwa kwa serikali kutekeleza mpango wa amani wa 2018.

Ilielezwa kuwa Sudan Kusini imekuwa na amani rasmi tangu makubaliano ya 2018 kumaliza mzozo wa miaka mitano uliosababisha vifo kwa maelfu ya watu, licha ya ghasia kati ya jamii hasimu huibuka mara kwa mara. **TRT**

HABARI MICHEZO

# MMILIKI KENGOLD AKIRI TATIZO NI KUFELI USAJILI, AAHIDI MAKUBWA

**Na Adam Fungamwango**

MMILIKI wa Klabu ya KenGold, Kenneth Mwakyusa, amekiri kuwa alifeli kwenye usajili wa dirisha kubwa kitu ambacho kimesababisha timu isifanye vema mpaka sasa, akiahidi kurekebisha hilo kipindi cha dirisha dogo Desemba na Januari mwakani.

Akizungumza jana kutoka jijini Mbeya, Mwakyusa alisema kufanya vibaya kwa timu yake kwa kiasi kikubwa kunatokana na kutokuwa na baadhi ya wachezaji wenye uwezo mkubwa na kwamba kitu hicho kilikosewa kwenye usajili.

**KenGold inacheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya kupanda, lakini kabla ya mchezo wao wa leo dhidi ya Yanga, tayari ilikuwa imepoteza mechi ya nne mfululizo ilichezocheza.**

Ilianza kwa kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Singida Black Stars, ikapoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Fountain Gate, ikadunguliwa bao 1-0 dhidi ya KMC, kabla ya kupata kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.

"Najua kwenye usajili nilifeli kidogo ndiyo maana tunapata matokeo haya, lakini najua kwenye dirisha dogo nitafanya vizuri, nitafanya usajili ambao utaifanya timu kuwa imara na tishio," alisema Mwakyusa.

Hata hivyo, pamoja na kuendelea kufanya vibaya, lakini amewataka wachezaji na benchi la ufundi kupambana na kusonga mbele, huku akiahidi kuendelea kufanya kila kitu kwa ajili ya timu hiyo ikiwamo kuwalipa wachezaji mishahara kwa wakati.

"Matokeo yaliyopita si ndwele, tugange yajayo, nawaahidi sitowaacha nitaendelea kuwaunga mkono kwa hali yoyote ile na kuwalipa mishahara, tayari mwisho wa mwezi unafika mishahara yao itafika wakati wowote," alisema.

Mwakyusa, ambaye ni mfanyabiashara wa madini, alianza kuimiliki timu hiyo kwa kuinunua Gipco FC ya Geita iliyokuwa Ligi ya Championship, na baada ya hapo akaibadilisha jina kabla ya kuanza kucheza ligi hiyo na kufanikiwa kupanda Ligi Kuu.

## TUPO PAMOJA...



Mashabiki wa Yanga, wakiipa mapokezi makubwa timu yao baada ya kutua jijini Mbeya tayari kwa mchezo wao wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa leo katika Uwanja wa Sokoine jijini humo, ambapo waliisindikiza hadi hotelini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yalia na marefa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MATOKEO ya sare tasa yameifanya Polisi FC kulia na waamuzi waliochezesha mechi yao dhidi ya Sebleni United kwa kueleza kuwa yamechangiwa na wao kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria 17 za soka.

Mchezo huo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja iliyoanza kutimua vumbi juzi, Jumatatu, ulichezwa kwenye Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Msaidizi wa Polisi FC, Yusuph Sape, alisema lazima waamuzi wawe makini katika utekelezaji wa majukumu yao hasa katika kutenda haki.

Alisema maamuzi yasio na usahihi yanachangia kwa kiasi kikubwa kuwavunja moyo wachezaji wawapo uwanjani, lakini pia hata kupoteza mashabiki kwenda viwanjani.

Kocha huyo alidai kuwa katika mchezo wao huo mwamuzi wa kati, Ramadhani Kessi, aliwanyima penalti mbili za wazi baada ya mshambuliaji wake kuangushwa eneo la hatari.

Alisema maamuzi ya waamuzi, muda mwingine yanachangia hata wachezaji kushindwa kujituma vizuri kuhakikisha timu yake inapata matokeo.

"Waamuzi wawe makini sana katika kufanya kazi zao, maamuzi yao hayaathiri timu pekee, bali soka lote hususan katika kupoteza wafuatiliaji na watazamaji," alisema.

Aidha, alisema kikosi chake kinahitaji kufanyiwa maboresho makubwa katika nafasi ya ushambuliaji pamoja na beki wa kati na kwamba ndizo idara ambazo ameona kuna tatizo kubwa katika mchezo huo wa kwanza.

Matokeo mengine ya ligi hiyo, katika Uwanja wa Cairo Kiwengwa, timu ya Ujamaa FC nayo iligawana alama dhidi ya Sharpboys baada ya kutoka sare ya bao 1-1.

# *Ouma aanika sababu kuondoka Coastal Union*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa zamani wa Coastal Union, David Ouma, amefunguka kuwa hakutimuliwa kazi kwenye klabu hiyo bali klabu hiyo ilishindwa kumpa mkataba mpya.

Hii ni mara ya kwanza kwa kocha huyo kufunguka tangu alipoondoka klabuni hapo akiipa mafanikio makubwa kwa mara ya kwanza kwa kucheza michuano ya kimataifa baada ya miaka 35.

Awali, ilielezwa kuwa kocha huyo alitimuliwa baada ya timu hiyo kuondoshwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuchapwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola licha ya kutoa suluhu nyumbani, lakini mwenyewe ameibuka na kusema klabu yake ilishindwa kumpa mkataba.

"Sijajua ni kwa nini, walishindwa kuniamini tena au gharama, lakini nilikuwa nimeshaonesha kazi ambayo haina shaka. Hata mwanzo nilipokuja hawakuniamini, wakataka kunipa mkataba wa mechi kadhaa, lakini niliwaambia wanipe tu mpaka mwisho wa msimu," alisema Ouma, straika wa zamani wa Timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars.

"Nilifika Coastal Union ikiwa nafasi ya 14, lakini nikaisukuma juu hadi ikamaliza nafasi ya nne na kukata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho la Soka Afrika, wakati naingia kila mmoja alikuwa amekata tamaa, kuanzia wachezaji hadi mashabiki, nikiwaeleza wasiwe na wasiwasi, nikawaeleza nitawatoa kwenye eneo la hatari, lakini kila mmoja aliona kama naota ndoto, kile nilichosimamia na kuwaahidi kikafanyika, nashangaa wameshindwa kunipa tena mkataba," alisema kocha huyo.

Alisema kwa sasa yupo na anaweza kuifundisha timu yoyote ile nchini, huku taarifa zikimhusisha na Klabu ya KenGold, ambayo pia Juma Mgunda anahusishwa kwenda huko kuinoa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GARETH ATAJWA EVERTON

MMILIKI mtarajiwa wa Everton, Dan Friedkin, amemtambua kocha wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate mwenye umri wa miaka 54, kama mtu anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Muingereza mwenzake Sean Dyche mwenye miaka 53, pale kwenye Uwanja wa Goodison Park. ***(GiveMeSport)***

### LIVERPOOL YASAKA NYOTA

LIVERPOOL inajiandaa kuivamia Bayer Leverkusen kwa kiungo wao wa Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa 21, mlinzi wa Uholanzi Jeremie Frimpong mwenye miaka 23, na kiungo wa kati wa Argentina Exequiel Palacios, 25. ***(CaughtOffside)***

### ZUBIMENDI NA LIVERPOOL

LIVERPOOL pia wana nia ya kumsajili kiungo wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, kutoka Real Sociedad katika msimu wa Januari wa usajili wa wachezaji. ***(Fabrizio Romano)***

### GOMEZ AWANIWA VILLA

MLINZI wa Liverpool na England, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na Klabu za Aston Villa na Newcastle United. ***(Football Insider)***

### MURILLO ATAKIWA MADRID

REAL Madrid inamfuatilia mlinzi wa Nottingham Forest, Murillo mwenye umri wa miaka 22, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona na Bayern Munich kumpata Mbrazil huyo. ***(HITC)***

### GOMES AZIVUTIA NYINGI

KLABU za Newcastle United, Manchester United na Tottenham Hotspur ni miongoni mwa zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Lille na England, Angel Gomes mwenye umri wa miaka 24. ***(GiveMeSport)***

### DIAZ KUONGEZA MKATABA

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya mazungumzo na winga wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27, kuhusu mpango wa kuongeza mkataba wake hadi 2027 kutokana na mwanzo wake mzuri wa msimu huu. ***(Football Insider)***

### LARSSON SASA AFUATILIWA

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt aliye na umri wa miaka 20 kutoka Sweden, Hugo Larsson. ***(Fabrizio Romano)***

### DIBLING ASHAWISHIWA

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(GiveMeSport)***

### CONNOLLY AWANIWA

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RODRI SASA KUKOSA MSIMU MZIMA CITY

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Rodri atakosa karibu msimu uliosalia baada ya vipimo Jumatatu asubuhi kupendekeza amepasuka kwenye goti lake la kulia wakati wa sare ya Jumapili dhidi ya Arsenal, chanzo kimeeiambia ESPN.

**Chanzo hicho kiliiambia ESPN kwamba mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania ana uwezekano wa kufanyiwa upasuaji huko Barcelona.**

Rodri alitolewa katika dakika ya 21 ya mechi hiyo ya Jumapili baada ya kushuka chini akiwa ameshika goti ikiwa ni mara yake ya kwanza kuanza Ligi Kuu msimu huu.

City walipata bao la kusawazisha dakika za mwisho kupitia kwa John Stones na kuambulia sare ya mabao 2-2 dhidi ya Arsenal kwenye Uwanja wa Etihad.

**Ni baada ya kuumia kwenye mechi ya Jumapili dhidi ya Arsenal na sasa atafanyiwa...**

Matokeo hayo yaliihakikishia timu hiyo ya Pep Guardiola kubaki kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi 13 katika michezo mitano ya kwanza waliyocheza.

Rodri alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa michuano ya Euro 2024 baada ya kucheza nafasi muhimu katika ushindi wa Hispania.

Ni miongoni mwa wanaopigiwa upatu kutwaa tuzo ya Ballon d'Or, na jeraha lake litakuwa pigo kubwa kwa City, ambao wanawinda taji lao la tano mfululizo la Ligi Kuu England.

Wiki iliyopita, Rodri aliweka wazi kuwa wachezaji "wako karibu" kugoma kutokana na wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa mzigo wao wa kazi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alicheza mechi 63 kwa klabu na taifa msimu uliopita katika kampeni ambayo haikukamilika hadi fainali ya Euro 2024 mnamo Julai 14.

Alipoulizwa kama ratiba hiyo ya kushtukiza inaweza kusababisha wachezaji kugoma, Rodri alisema: "Nadhani tunakaribia hilo; ni rahisi kuelewa. Nadhani ni jambo la jumla. Nadhani ukimuuliza mchezaji yeyote, atasema vivyo hivyo - si maoni ya Rodri au chochote.

"Nadhani ni maoni ya jumla ya wachezaji. Na ikiwa itaendelea hivi, kutakuwa na wakati ambapo hatutakuwa na chaguo lingine, ninafikiria sana, lakini wacha tuone. Sijui nini kitatokea, lakini ni jambo ambalo linatutia wasiwasi kwa sababu sisi ndio watu wanaoteseka."

## HABARI MICHEZO

# BARCA KUSAJILI KIPA MBADALA WA TER STEGEN



**BARCELONA,** Hispania

UONGOZI wa Barcelona utafanya mazungumzo ya dharura wiki hii kujadili iwapo watamsajili kipa atakayechukua nafasi ya Marc-Andre ter Stegen ambaye ni majeruhi, vyanzo viliiambia ESPN.

Ter Stegen mwenye umri wa miaka 32, alifanyiwa upasuaji uliofanikiwa Jumatatu, ambapo Barca ilisema ni baada ya kupasuka kabisa mshipa wa goti lake la kulia katika ushindi wa mabao 5-1 wa LaLiga Jumapili dhidi ya Villarreal.

Vyanzo vimeiambia ESPN kipa huyo wa Ujerumani atakuwa nje ya uwanja kwa miezi kadhaa na hakuna uwezekano wa kucheza tena msimu huu.

Inaki Pena aliingia kuchukua nafasi yake. Alicheza mechi 12 kwenye LaLiga msimu uliopita huku Ter Stegen akiwa nje kwa tatizo la mgongo.

Lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Kocha wa Barca, Hansi Flick, Mkurugenzi wa Michezo Deco, na maofisa wengine wa ngazi ya juu wa klabu watakutana ili kuchambua jinsi ya kuendelea bila Ter Stegen.

Chaguo ni kuambatana na Pena, kusajili kipa ambaye hana klabu ya kushindana na mhitimu wa akademi au kusubiri hadi dirisha la uhamisho la Januari litakapofunguliwa ili kutathmini hali hiyo.

Kanuni za LaLiga zitairuhusu Barca kusajili mchezaji huru nje ya dirisha la uhamisho kutokana na jeraha la muda mrefu alilopata Ter Stegen.

Klabu ya hiyo ya Katalunya imesalia kuvuka kiwango cha matumizi ya kila mwaka kilichowekwa na ligi - ingawa imepanda hadi zaidi ya euro milioni 400, lakini itaruhusiwa kuwekeza hadi asilimia 80 ya mshahara wa Ter Stegen badala yake.

Ni sheria ambayo tayari Barca wametumia msimu huu kumsajili Inigo Martinez, Dani Olmo na Pau Victor kwenye LaLiga kutokana na majeraha ya Ronald Araújo na Andreas Christensen.

Keylor Navas, Loris Karius na mchezaji wa zamani wa Barca, Jordi Masip, ni miongoni mwa makipa ambao kwa sasa hawana klabu ambao wanaweza kusaini mara moja.



# Haaland aepuka adhabu mechi Arsenal

**MANCHESTER,** England

ERLING Haaland hatakabiliwa na adhabu kwa kumtupia mpira Gabriel Magalhaes baada ya bao la dakika za lala salama la Manchester City dhidi ya Arsenal, chanzo kiliiambia ESPN.

Kamera zilimnasa Haaland akirusha mpira nyuma ya kichwa cha mlinzi wa Arsenal baada ya John Stones kufunga na kufanya mabao kuwa 2-2 kwenye Uwanja wa Etihad Jumapili.

Tukio hilo halikuonwa na mwamuzi wa uwanjani Michael Oliver, lakini lilionekana na mwamuzi msaidizi wa video, John Brooks, ambaye aliamua kuwa haikuwa tabia ya vurugu.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba FA inafurahi kwamba tukio hilo lilishughulikiwa wakati huo na Haaland hatakabiliwa na hatua za kinidhamu.

Haaland, ambaye alifunga na kuifanya City kuwa mbele kwa bao 1-0 mapema kwenye mchezo huo, alihusika katika majibizano makali na Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta na mshambuliaji Gabriel Jesus baada ya filimbi ya mwisho.

Wachezaji wa City walikasirishwa na kile walichokiona kuwa kupoteza muda na Arsenal walipojaribu kucheza kipindi cha pili wakiwa na wachezaji 10 baada ya kutolewa kwa Leandro Trossard kwa kadi nyekundu.

Kamera za Sky Sports pia zilirekodi Haaland akigombana na Jesus baada ya filimbi ya mwisho baada ya kumwambia Arteta "akae mnyenyekevu" huku kocha wa Arsenal akipeana mikono na wachezaji uwanjani.

"Kuwa mnyenyekevu, eh; kuwa mnyenyekevu, eh," mchezaji huyo wa Kimataifa wa Norway alimwambia kocha wa Arsenal, ambaye hakujibu. Wakati wa mabishano makali na Jesus.

# Mourinho akejeliwa na Galatasaray

**ISTANBUL,** Uturuki

KOCHA wa Fenerbahce, Jose Mourinho, ameitwa "mliaji" na Galatasaray baada ya timu yake kupoteza kwa mabao 3-1 nyumbani katika mchezo wao dabi ya Istanbul juzi.



Kilikuwa kipigo cha kwanza kwa Fenerbahce katika Super Lig msimu huu na kuwaacha vijana wa Mourinho wakiwa nyuma ya Galatasaray kwa pointi tano.

Mourinho, ambaye alijitambulisha kama 'Special One' katika kipindi chake cha kwanza Chelsea, aliondoka uwanjani bila kuhudhuria mkutano wa wanahabari baada ya mchezo huo.

Galatasaray ilichapisha kwenye akaunti yao rasmi ya X picha yenye jina "The Crying One" iliyoandikwa kwa Photoshop, ikiwa na picha ya Mourinho akiwa na huzuni kwenye jalada hilo.

Klabu hiyo pia ilichapisha picha ya Mourinho nyuma ya kocha wa Galatasaray Okan Buruk wakati wa mchezo ikiwa na nukuu "mshindi."

Mourinho, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa Fenerbahce majira ya joto, miezi sita baada ya kutimuliwa Roma, hivi majuzi alijiita 'The Foreign One' aliposhughulikia hitaji lake la kuzoea soka la Uturuki.

Kocha huyo Mreno anajaribu kuiongoza Fenerbahce kutwaa taji lao la kwanza la Super Lig ndani ya muongo mmoja.

Fenerbahce watarejea uwanjani Alhamisi kuwakaribisha Royale Union Saint-Gilloise katika mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Europa.

HABARI MICHEZO

# TPLB NA SABABU SIMBA, AZAM FC KUPIGWA ZENJI

Na Adam Fungamwango

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imeutaja Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuwa sababu ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Azam na Simba kupelekwa Zanzibar, badala ya kuchezwa Bara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, alisema mechi hiyo imepelekwa huko kwa sababu kadhaa, ikiwamo wamiliki wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao ni serikali kutoruhusu mchezo wa ligi kwa sasa kutokana na kuendelea kwa matengenezo, lakini pia msimu huu kanuni zinaruhusu mechi kupigwa Zanzibar.

**Azam itaikaribisha Simba, kesho kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, ambao utaingia kwenye kumbukumbu ya kuwa mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kupigwa Zenji.**

Kasongo alisema awali Azam ilikuwa icheze mechi yake hiyo Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini baada ya kutoruhusiwa kwa sasa ndipo walipowaandikia barua ya kutaka kuupeleka mjini Zanzibar.

"Tulitetewa barua na Azam kuomba mchezo wao kuchezwa Uwanja wa New Amaan Zanzibar, awali waliomba kutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa katika michezo yao miwili ikicheza na timu za Simba na Yanga, badala ya kuichezea Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Lakini kutokana na mazingira ya uwanja jinsi yalivyo, wamiliki wameshindwa kuwaruhusu, kwa hiyo wakaomba Uwanja wa New Amaan, na kwa sababu msimu huu kanuni zinaruhusu hilo, hakuna sehemu inayozuia kutumia viwanja vya Zanzibar kwa ajili ya michezo yetu ya Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship na 'First League,'" alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Kumekuwa na mageuzi makubwa msimu huu kwenye soka la Tanzania, kwani mechi ya Ngao ya Jamii ilipigwa Zanzibar katika Uwanja huo, Agosti 8, mwaka huu, kwa mara ya kwanza, lakini kama vile haitoshi, Yanga ilicheza mchezo wake wa marudiamo, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE kwenye uwanja huo.

## Mo auona ubingwa wa CAF Simba

INATOKA UK. 24

tayari Klabu ya Simba inasemekana imemalizana na winga, Elie Mpanzu, ambaye kwa sasa amemaliza mkataba wake na AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na alionekana katika mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya akishangilia ushindi wa mabao 3-1 Simba iliyoupata Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kutinga hatua ya makundi.

Wakati huo, mchezaji wa timu hiyo, Edwin Balua, amekiri kuwa mchezo huo ulikuwa na presha mno si kwa mashabiki pekee, bali pia wachezaji.

Balua ambaye alifunga bao la tatu lililowashusha presha mashabiki wa Simba, alisema ndiyo maana alivua jezi baada ya kufunga kwani alijua hakuna tena kitu ambacho kingewazuia kufuzu hatua ya makundi.

"Mechi ilikuwa ngumu na presha, tulikuwa tunacheza huku tukijua kabisa kuwa kama wakirudisha tu basi mzigo mkubwa utakuwa kwetu, na inawezekana tukashindwa kuingia kwenye hatua ya makundi, kwa hiyo tulicheza kwa tahadhari mno na presha kubwa hasa kile kipindi ambacho tunaongoza mabao 2-1 na dakika zinayoyoma.

"Wenzetu wanaona wahamie kabisa langoni mwetu na kusaka bao la kuwavusha, kwa bahati ikapatikana nafasi ile nikaenda kufunga, kusema kweli furaha ilikuwa kubwa sana, nilijua basi tumeshafuzu, ndiyo maana nilivua jezi kwa sababu ya furaha," alisema Balua.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema baada ya kumalizika kwa hatua hiyo, akili na nguvu zao sasa wanazielekeza katika mchezo wa kesho dhidi ya Azam FC, utakapopigwa, Uwanja wa New Amaan Complex, mjini Zanzibar.

Simba imeshacheza michezo mwili ya Ligi Kuu mpaka sasa, ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Tabora United na 4-0 dhidi ya Fountain Gate.



Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya KenGold utakaopigwa leo katika Uwanja wa Sokoine, Mbeya. **MPIGAPICHA WETU**

## Yanga yaigeukia KenGold Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

kinyonge," Kamwe alisema.

Aliongeza kuwa anajua KenGold ina kikosi kizuri na matokeo waliyopata katika michezo iliyotangulia hayatokani na kucheza vibaya bali anaamini hawakuwa na bahati ya kupata ushindi.

Katika kuhamasisha mashabiki wao kufika kuishangilia timu yao, leo asubuhi wataanza na zoezi la kunywa supu.

"Hili sasa tutakuwa tunalifanya katika kila mkoa ambao tunaenda kucheza, safari hii tutakunywa supu na ubwabwa, lakini tu nipende kuwaambia mashabiki wetu Yanga imerejea katika Ligi Kuu na kasi yake ile ile ya kusaka ushindi," alisema ofisa huyo.

Kocha Mkuu wa KenGold, Jumanne Chale, alisema wachezaji wake wako tayari kuelekea mechi ya leo na anaamini wataongeza umakini na kufuata maelekezo yake vema ili kuibuka na ushindi.

Chale alisema Yanga isitarajie mteremko kueleea mechi hiyo kwa sababu wamewafuatilia na kujua mapungufu yao.

Mmiliki wa timu hiyo, Kenneth Mwakyusa, amekiri hakufanya usajili mzuri na ameahidi kurekebisha makosa yake wakati wa dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa.

"Nimekutana na wachezaji na kuzungumza nao ili kuweka mambo sawa, tunaelekea mwisho wa mwezi, nimewaeleza watapata mishahara yao kwa wakati na wajipange kutupa matokeo mazuri," alisema Mwakyusa.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya wenyeji, JKT Tanzania dhidi ya Coastal Union kutoka Tanga.

## *Pamba Jiji yawatuliza mashabiki wake*

Na Somoe Ng'itu

KUTOKANA na timu yao kuwa na matokeo ya kusuasua katika Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Pamba Jiji FC, umewataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kuwa watulivu kwa sababu muda bado upo wa kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chao.

Pamba Jiji ina pointi nne kibindoni baada ya kushuka dimbani mara tano katika ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Pamba Jiji, Biku Kotecha, alisema mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na wachezaji wao wamekuwa wakipambana kusaka matokeo chanya na wanachokipata ni kutokana na kucheza kwa juhudi.

Kotecha alisema wanaendelea kurekebisha mapungufu na anaamini mechi zinazofuata watapata ushindi kwa sababu wachezaji wao wameanza kuzoea 'joto' la Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunawaomba mashabiki wetu wasikate tamaa, muda bado upo, hii ni Ligi Kuu, ushindani wake ni mkubwa zaidi, lakini hata ukiangalia msimamo utaona timu zimepishana pointi chache," alisema Kotecha.

Pamba Jiji ambayo huu ni msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu katika kipindi cha miaka 23, tangu iliposhuka daraja mwaka 2001, itarusha tena karata yake dimbani kwenye mwendelezo wa ligi hiyo, Septemba 28, mwaka huu, kwa kuwavaa wenyeji wao, Coastal Union ya jijini Tanga, Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

# Michezo

Jumatano Septemba 25, 2024

Nipashe




Barca kusajili mbadala wa Ter Stegen UKURASA 22

# YANGA SC YAIGEUKIA KENGOLD

## ●●● Gamondi aahidi mabadiliko akiwataka wachezaji wake kurudisha akili na mawazo...

**Somoe Ng'itu na Faustine Feliciane**

HATUTAWADHARAU, hayo ni maneno ya Mabingwa Watetezi, Yanga, kutoka Dar es Salaam kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KenGold itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

**Yanga itashuka dimbani katika mchezo huo ikitoka kutoa kipigo kikubwa cha mabao 6-0 dhidi ya CBE ya Ethiopia kwenye mechi ya marudiano ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Matokeo hayo na yale ya mechi ya awali ugenini nchini Ethiopia ya ushindi wa bao 1-0 wiki moja kabla, yameifanya Yanga kufuzu hatua hiyo ya makundi kwa jumla ya mabao 7-0, hivyo kusubiri droo ya makundi itakayochezeshwa jijini Cairo, Misri Oktoba 7, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema timu yake imejiandaa kucheza soka la ushindani kwa sababu wanakutana na timu mpya inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza.

Gamondi alisema anatarajia kukutana na ushindani kwa sababu wanacheza dhidi ya timu hiyo, hivyo kila upande utahitaji kumsoma mpinzani wake wakati inahitaji kufanya mashambulizi.

Kocha huyo alisema anawaheshimu KenGold kwa sababu ni moja ya timu zilizoonesha kiwango bora walipokuwa wanashiriki Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), hivyo hawatawadharau.

"Hatutarajii mchezo mwepesi, tutaingia uwanjani kupambana kusaka ushindi, tunahitaji pointi tatu ili kuendelea na safari yetu ya kutetea ubingwa," alisema Gamondi.

Alisema wachezaji wake wote wako katika hali nzuri na wanatarajia kuhamishia morali ya mashindano ya Kimataifa ya CAF katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Aidha, Gamondi aliwataka wachezaji wake sasa kugeukia michezo ya Ligi Kuu baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya makundi kwa kuitupa nje ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa CBE ya Ethiopia.

Alisema sasa wanatakiwa kusahau kwa muda Ligi ya Mabingwa na kugeukia michezo yao ya Ligi Kuu.

"Mchezo hautakuwa mwepesi, kuna tofauti katika maandalizi ya michezo ya kimataifa na hii ya ligi, nimewataka wachezaji wangu kusahau mambo ya Ligi ya Mabingwa...., akili zetu tuzielekeze kwenye Ligi Kuu," alisema Gamondi.

Aidha, alisema kuwa ataendelea kuwafanyia mabadiliko wachezaji wake ili kutoa nafasi ya kuwapumzisha baadhi ya nyota wake kutokana na ratiba kuwabana.

"Kikosi changu kitakuwa kikibadilika badilika kulingana na aina ya mpinzani tunayecheza naye, jambo zuri nina kikosi kipana na wachezaji wenye ubora, hii itatusaidia kukabiliana na ratiba ngumu mbele yetu," alisema Gamondi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wanatarajia kukutana na ushindani kwa sababu kila upande unataka kuondoka na alama tatu muhimu kutoka kwenye mechi hiyo.

Kamwe alisema kwao hakuna timu ndogo na wamejipanga kuwapa furaha mashabiki wao kwa kuwapa ushindi.

"Huku katika Ligi Kuu ya NBC ni pagumu zaidi, tunacheza na timu tunayojuana, tutacheza kwa tahadhari. Tunataka kuendelea pale tulipoishia, hatutawadharau KenGold, tunawaheshimu kwa sababu nao wamejiandaa na hawataingia

INAENDELEA UKURASA 23

KUNA SWALI?...



Winga wa Simba, Edwin Balua, aliyeipeleka hatua ya makundi Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kupigilia nyundo ya mwisho wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya katika Uwanja wa Benjamin Mkapa mwishoni mwa wiki. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Mo auona ubingwa wa CAF Simba

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Heshima na Mwekezaji wa Simba, Mohamed Dewji, amesema kikosi cha timu hiyo kina uwezo wa kufanya vema, ikiwamo hata kutwaa Kombe la Shirikisho kama nguvu itaongezwa kidogo, huku ahadi yake ya kuiona timu hiyo ikitwaa Ubingwa wa Afrika ukiwa pale pale.



Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mo alisema kikosi cha msimu huu kimeanza kurejesha heshima ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwani wachezaji wanaonekana kujali na kuipigania nembo ya Simba, na nguvu ikiongezwa kidogo wana uwezo mkubwa wa kutwaa Kombe la Shirikisho Afrika ambalo tayari wameingia makundi.

Alisema wachezaji wanaoonekana kwenye kikosi hicho wengi ni vijana ambao hawana uzoefu sana kwenye michuano ya kimataifa, lakini wanacheza kwa kupambana, kupigania nembo ya klabu kwa kuvuja na kuacha jasho lao lote uwanjani, kitu ambacho kilikosekana kwenye miaka michache nyuma, huku akitarajia kuwa kitafanya makubwa msimu ujao wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Nimefurahi sana, kikosi kiko vizuri na kama kikiendelea kucheza hivi, nguvu ikaongezwa kidogo hiki hiki kinaweza kutwaa Kombe la Shirikisho Afrika, na kwa hivi tunavyokwenda naona matarajio yangu hayako mbali sana.

"Matarajio yangu ni yale yale, miaka sita iliyopita nilisema nataka kuona Simba inatwaa ubingwa wa Afrika, lakini watu wakanicheka, furaha yangu ni kuona timu yangu inatwaa ubingwa wa Afrika kwa hiki ninachokiona hatupo mbali sana, hiki kikosi msimu ujao kikiingia Ligi ya Mabingwa kitawashangaza wengi, wachezaji hawa watakuwa tayari wameshapata uzoefu na wameiva," alisema.

Wakati Mwenyekiti huyo wa Bodi ya Wakurugenzi akizungumza hayo,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >